**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

---

**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**
**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

***ZANZIBAR*** ***APRILI, 2022***

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**



**MHE. HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**



**MHE. HAMZA HASSAN JUMA**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**(SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI)**



**ND. THABIT IDAROUS FAINA**
**KATIBU MKUU OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**(SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI)**

## Dira:

*“Kuwa na Serikali yenye kutoa huduma bora kwa jamii na yenye uhimili mzuri wa uchumi, umoja na maendeleo endelevu”.*

## Dhamira

*“Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zote za SMZ na masuala ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kufuata misingi ya haki za binaadamu na ushirikishwaji”.*

## YALIYOMO

YALIYOMO....................ii
UTANGULIZI....................1
PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS....................27
PROGRAMU KUU - ((PCO102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI....................29
PROGRAMU KUU - (PCO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS....................41
PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU – PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI....................47
TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)....................48
PROGRAMU KUU - (PCO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI....................48
PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR....................50
UTEKELEZAJI KIFEDHA....................51
MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023....................52
PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS....................52
PROGRAMU KUU - (C0102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI..54
PROGRAMU KUU - (CO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS....................61
PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI na PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI....................65
PROGRAMU KUU - (CO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI....................67
PROGRAMU KUU - (CO301): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR....................67
UKUSANYAJI MAPATO....................68

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### Utangulizi

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijaendelea na hotuba hii, nachukua nafasi hii kumshuruku Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema pamoja na kutuwezesha kufunga Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan katika hali ya salama na amani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake atuwezeshe kuumaliza Mwezi huu na atukubalie swaumu zetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** hatunabudi pia kumshukuru Muumba wetu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana tena hapa leo kwa ajili ya kuwasilisha na kujadili taarifa za utekelezaji za mwaka 2021/2022 na mipango ya Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

4. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kuiongoza nchi yetu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa taifa letu. Aidha, kwa dhati kabisa nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake imara uliojaa hekima na busara na wenye azma kubwa ya kuiletea Zanzibar maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

5. **Mheshimiwa Spika,** bila shaka sote ni mashuhuda wa kazi nzuri wanazozifanya viongozi wetu hawa ya kujenga misingi imara ya kuleta maendeleo katika nyanja zote. Uongozi wao thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri zinazofanywa na Serikali zetu zote mbili kwa kushirikiana na wananchi wote. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo, afya na hekima zaidi katika uongozi wao pamoja na sisi sote tunaowasaidia.

6. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, kwa upekee kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa namna unavyoliongoza Baraza hili kwa kushirikiana na Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza. Hakika uongozi wenu katika kusimamia shughuli zote za Baraza umekuwa na mafanikio makubwa. Vilevile, nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi kwa namna wanavyoendelea kutimiza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi wakati wakiwa katika maeneo yao, wanapokuwa katika Vikao vya Baraza lakini pia wanavyokuwa katika Kamati za Kudumu za Baraza. Kwa kweli Baraza letu hili limeisaidia sana Serikali katika utoaji wake wa huduma kwa wananchi kutokana na maelekezo na ushauri unaotolewa mara kwa mara.

7. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya shukurani na pongezi, kwa ridhaa yako sasa naomba nieleze kwa muhtasari hali halisi ya masuala mbalimbali ya kisekta na kitaifa yaliyofanyika au yaliyopangwa kufanywa katika nchi yetu. Masuala hayo yataelezwa kwa undani zaidi na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika wakati watakapowasilisha hotuba zao za bajeti.

**Hali ya Kisiasa**

8. **Mheshimiwa Spika,** hali ya kisiasa katika nchi yetu inaendelea kuwa ni ya utulivu na tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujaalia neema hii. Bila shaka hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na uendeshaji wa Serikali

yetu unaofuata misingi ya haki na maridhiano kama ilivyoelekezwa na Katiba yetu. Wananchi wameendelea kuishi kwa kushirikiana na kuonesha umoja katika harakati zao za kujiletea maendeleo. Hali hii ya kisiasa tuliyonayo pia inasaidia sana katika kujenga jamii tunayoitaka inayoishi kwa mshikamano na kuimarisha udugu wetu. Hivi sasa Zanzibar imekuwa mfano kwa mataifa mengine kutokana na namna inavyoendesha shughuli zake za kisiasa na kiserikali. Hali hii pia imekuwa ni msingi mkubwa wa kudumisha umoja na mshikamano wetu na kutoa fursa kwa wananchi kutumia haki ya kikatiba ya kushiriki katika shughuli zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar; Kwanza tuendelee kuwa na mshikamano katika kuiletea Zanzibar maendeleo; Pili, kila mmoja wetu atambue umuhimu wa kuvumiliana, kustahimiliana na kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha amani na utulivu katika nchi yetu kwa kuacha vitendo na maneno ya kichochezi ambayo bila shaka hayatokuwa na tija kwa ustawi wetu. La tatu ni kuendelea kujitolea na kuimarisha uzalendo katika nchi yetu pamoja na kujenga imani ya hali juu kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Hali ya Uchumi wa Zanzibar**

**Hali ya Ukuaji wa Uchumi**

10. **Mheshimiwa Spika,** kasi ya Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar imeimarika na kufikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2020. Ukuaji huo wa Uchumi kwa mwaka 2021 umetokana na kupungua kwa kasi ya maambukizi ya maradhi ya UVIKO-19 duniani. Sekta zilizoimarika zaidi ni sekta ya huduma kwa kufikia ukuaji wa asilimia 6.8 kutoka asilimia -1.0 ya mwaka 2020 kulikotokana na kuimarika kwa shughuli za utalii; kuimarika kwa sekta ya fedha kufikia asilimia 9.9 kutoka asilimia 2.1; kuimarika kwa shughuli za uwekezaji kulikopelekea kuongezeka kwa shughuli za ujenzi kufikia asilimia 8.9

kutoka asilimia 6.5; na kuimarika kwa sekta ya Umeme na Gesi kufikia asilimia 8.0 kutoka asilimia -2.8.

**Pato la Taifa na Pato la Mwananchi**

**11.** **Mheshimiwa Spika,** thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma imeongezeka hapa nchini na kufanya Pato halisi la Taifa kukua na kufikia thamani ya **Shilingi Trilioni 3.275** mwaka 2021 ikilinganishwa na thamani ya **Shilingi Trilioni 3.116** mwaka 2020. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za soko (GDP at Current Prices) limefikia thamani ya **Shilingi Trilioni 4.633** mwaka 2021 kutoka thamani ya **Shilingi Trilioni 4.209** mwaka 2020. Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumesababisha kuongezeka kwa Pato la Mwananchi na kufikia **Shilingi Milioni 2.7** ambazo ni sawa na **Dola za Kimarekani 1,171** kutoka **Shilingi Milioni 2.5** sawa na **Dola 1,099** kwa mwaka 2020. Kipato hiki kimeifanya Zanzibar iendelee kubaki katika nchi za uchumi wa kiwango cha kati cha chini (Low Middle-Income Status).

**Mfumko wa Bei**

**12.** **Mheshimiwa Spika,** kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imepungua na kufikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2020. Kupungua huko kumesababishwa na hatua za Serikali za kupunguza kodi za bidhaa za vyakula zikiwemo sukari, mchele na unga wa ngano kwa kiwango cha **Dola 350** kutoka **Dola 600** kwa kila tani moja na Serikali kutoa bei elekezi za bidhaa mbalimbali zilizoingia nchini ikiwemo bidhaa ya saruji na nondo. Hata hivyo, kwa mwaka 2022 kasi ya mfumko wa bei imeanza kupanda na kufikia asilimia 2.8 mwezi wa Januari na asilimia 2.9 mwezi wa Februari. Hii imetokana na kupanda kwa gharama za mafuta duniani.

***Usafirishaji na uagizaji wa bidhaa nje ya nchi***

13. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kufikia **Shilingi Bilioni 155.6** mwaka 2021 kutoka **Shilingi Bilioni 65.7** mwaka 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 136.8.** Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kufikia **tani 6,775.5** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 115.3** mwaka 2021 kutoka **tani 3,506.8** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 38.3** mwaka 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 93.2** la usafirishaji wa karafuu. Aidha, usafirishaji wa zao la mwani umeongezeka kufikia **tani 12,611.1** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 11.9** mwaka 2021 kutoka **tani 11,382.6** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 11.7** mwaka 2020. Kwa upande mwengine, uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 847.4** mwaka 2020 na kufikia **Shilingi Bilioni 968.6** kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 14.3.**

**Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2022**

14. **Mheshimiwa Spika,** kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022 kutoka asilimia 5.1 ya mwaka 2021 kutokana na sababu zifuatazo:

   i. Kupatikana kwa fedha za mkopo nafuu kutoka IMF na mkopo maalum kutoka Benki Kuu ya Tanzania;

   ii. Kuendelea kuongezeka kwa uingiaji wa watalii na kukadiriwa kufikia watalii 450,213 kwa mwaka 2022 ikiwa mgogoro wa Ukraine na Urusi utamalizika mapema;

   iii. Matarajio ya kuongezeka kwa mapato ya ndani kwa asilimai 7 kutokana na utekelezaji wa mikakati iliyopangwa na Serikali;

   iv. Kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji viwandani, ikiwemo uwekezaji mkubwa kwenye visiwa vidogo

vidogo, uzalishaji wa nguo kutoka Kiwanda cha Basra, Kiwanda cha Maji Chamanangwe na Kiwanda cha Viatu cha Amani;

v. Kuimarika kwa shughuli za kibiashara hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo baada ya upatikanaji wa fedha za mkopo nafuu;

vi. Kudhibiti matumizi ya Serikali na upotevu wa mapato kutokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa fedha na kuelekeza matumizi hayo katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

**Maendeleo ya Utalii**

**15.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha Sekta ya Utalii ili iweze kuongeza pato letu la taifa na kuongeza ajira kwa vijana wetu. Serikali inatekeleza mipango yake hiyo kwa kuweka mazingira bora na salama kwa watalii wetu sambamba na kuongeza vivutio vipya vya utalii hapa nchini.

**16.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanzisha kikosi kazi maalumu cha Polisi Utalii na Diplomasia ambacho kinahusika na kuhakikisha usalama wa watalii na mali zao wanapokuwa katika maeneo mbalimbali ya kitalii hapa nchini. Kwa sasa kikosi hicho kina jumla ya Maafisa Polisi 150 wanaotoka katika vikosi vyetu vya ulinzi na usalama. Kikosi hicho kimezinduliwa rasmi tarehe 19 Novemba, 2021 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ni mategemeo yetu kuwa kuimarika kwa ulinzi na usalama wa watalii wetu hawa kutaongeza shauku ya watalii hao kuja Zanzibar kwa mara nyengine sambamba na kuwashawishi wengine kuitembelea Zanzibar.

**17.** **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni tumeshuhudia zoezi la uchukuaji wa filamu ya "Royal Tour" ambayo imewashirikisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Filamu hiyo ambayo inaonesha fursa zilizopo Tanzania ikiwemo Zanzibar katika nyanja ya Uwekezaji, Utalii na Uhusiano wa Kimataifa inatarajiwa kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kimataifa.

18. **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza idadi ya watalii, vilevile Serikali imeongeza idadi ya kampuni za ndege zinazofanya safari kuja Zanzibar. Zanzibar tayari inapokea ujio wa ndege 34 ambazo zinafanya safari kutoka nchi zao na kufikia Zanzibar. Aidha, katika kipindi hiki cha Julai hadi Machi 2021/2022, Zanzibar imepokea jumla ya ndege 5 mpya zinazosafirisha watalii ambazo ni Air France, Azuri Air, Edelweiss, Global Air ways na Eurowings.

19. **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha mwaka 2021 imeongezeka kwa asilimia 51.2 na kufikia watalii 394,185 kutoka watalii 260,644 walioingia nchini mwaka 2020. Nchi zilizoingiza watalii wengi zaidi katika mwaka 2021 ni Urusi watalii 70,445 (17.8%), Ufaransa watalii 37,439 (9.5%), Poland watalii 36,925 (9.4%), Afrika ya Kusini watalii 19,936 (5.1%), Ujerumani watalii 16,670 (4.2%), Ukraine watalii 14,751 (3.7%), Uingereza watalii 11,571 (2.9%), Ubelgiji watalii 9,353 (2.4%) na nchi nyengine zilizosalia zimeingiza watalii kwa asilimia 45. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kumesababishwa na kuendelea kudhibitiwa kwa maambukizi mapya ya maradhi ya UVIKO-19 na kupungua kwa masharti kwa wasafiri pamoja na masoko makubwa ya utalii kufunguliwa na kuruhusiwa kwa safari za ndege.

**Uchumi wa Buluu**

20. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, imeweka misingi imara ya kuendeleza sekta ya Uchumi wa Buluu kwa maendeleo ya uchumi

wa Zanzibar. Sekta hii imedhamiria kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika Sekta ya Biashara na Viwanda ambayo itasaidia upatikanaji wa ajira kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia azma hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti katika kutoa elimu na uwezeshaji, usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari, utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari, ujenzi wa miundombinu, kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya baharini, upatikanaji wa masoko katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa Rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia.

22. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na sekta binafsi itatekeleza programu na miradi ya ujenzi wa miundombinu ya uvuvi ikiwemo ujenzi wa bandari, masoko, vyumba vya baridi pamoja na kuanza utaratibu wa ununuzi wa meli kubwa ya kisasa ya uvuvi pamoja na kukamilisha ugawaji wa boti 577 ambazo Serikali imeshaingia mkataba na Wakandarasi na kwa sasa zinaendelea kutengenezwa.

23. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa samaki kwa asilimia 18 kutoka **tani 38,000** mwaka 2020 hadi **tani 47,000.** Kutokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuwahudumia wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini, kiwango cha uvuvi kinatarajiwa kuongezeka tena kutoka **tani 47,000** mwaka 2021 hadi tani **60,000** kufikia Disemba 2022.

24. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imejipanga kuwawezesha wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kwa kuwapatia mafunzo na zana za kilimo cha mwani na imepanga kutoa jumla ya boti 500 na mashine za kusarifia mwani ikiwa ni sehemu ya mkakati wa muda mfupi wa

kukabiliana na tatizo la uzalishaji mdogo wa mwani. Aidha, ili kutatua suala la bei ndogo na soko dhaifu la mwani, Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani kitakachojengwa huko Chamanangwe Pemba. Kutokana na ujenzi huo, tunategemea kumaliza kabisa tatizo la bei ndogo ya mwani hapa nchini.

**Sekta ya Kilimo**

**25.** **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ni pamoja na kuimarisha Sekta ya Kilimo inayojumuisha sekta ndogo za mazao, mifugo na misitu. Sekta hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika ustawi wa wananchi wetu kwani ni moja ya sekta inayochangia kwa kiasi kikubwa utoaji wa ajira ambapo inachangia kwa wastani wa asilimia 40.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaimarisha huduma za umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya kisasa na kuacha kutegemea misimu ya mvua hasa kwa kilimo cha mpunga. Serikali tayari imekamilisha uchimbaji na ujenzi wa misingi ya umwagiliaji yenye urefu wa mita 1,400 katika bonde la Mlemele; uwekaji wa pampu katika visima 20 vya mabonde ya Cheju; Kibokwa na Kilombero. Ni mategemeo yetu kuwa kuwepo kwa miundombinu hiyo kutaongeza uzalishaji wa zao la mpunga kwa kiasi kikubwa na hivyo kuongeza kipato kwa wakulima wetu pamoja na kurahisisha upatikanaji wa zao hilo ambalo ndio chakula kikubwa hapa Zanzibar.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yetu inayosimamia masuala ya kilimo imeendelea kutoa huduma za ugani kwa wakulima wetu ikiwemo kutoa maelekezo juu ya njia bora za kilimo kwa mazao tofauti na sehemu tofauti. Zaidi ya wakulima 2,297 (713 Unguja na 1,584 Pemba) walitembelewa na mabwana na mabibi shamba na kupatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya shughuli zao za kilimo wanazozifanya. Aidha, jumla ya wakulima 19,888 walipatiwa mafunzo ya uzalishaji wa mboga mboga, kupunguza upotevu wa mazao,

mbinu za kilimo bora na kilimo hai. Haya yote yanalenga katika kuwafanya wakulima wetu kuweza kufaidika na shughuli zao za kilimo kwa kupata mazao mengi zaidi na yaliyo katika hali ya ubora ili kupata bei inayoridhisha na kukidhi mahitaji yao.

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maliasili zetu ikiwemo misitu, Serikali imeendelea kuwahamasisha wananchi kuhifadhi maliasili zetu kwa kuendelea kuitunza misitu na kupanda mingine katika maeneo mbalimbali. Serikali imeendelea kuotesha miche kwa ajili ya wananchi kuweza kuipata kwa urahisi na kuipanda. Jumla ya miche 511,727 ilioteshwa katika vitalu mbalimbali vya Serikali Unguja na Pemba ikijumuisha miche 400,430 ya misitu, miche 105,922 ya matunda na miche 5,375 ya viungo.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuitunza na kuihifadhi rasilimali hii ya misitu, Serikali inaendelea kufanya doria katika maeneo mbalimbali ambapo jumla ya doria 243 (200 Unguja na 43 Pemba) zimefanywa. Doria hizi kimsingi zinasaidia sana katika utunzaji huo kwani katika kipindi hiki kumeripotiwa matukio 45 (25 Pemba na 20 Unguja) ya uharibifu wa makusudi wa misitu yetu. Serikali itaendelea kuchukua hatua hizi na watakaokamatwa wataendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maendeleo ya mifugo, Serikali vile vile inaendelea kutoa huduma za ugani kwa wafugaji wetu ili kuwawezesha kupata tija kutokana na shughuli zao za ufugaji. Jumla ya wafugaji 5,444 wakiwemo wafugaji wa ng'ombe 3,062, wa mbuzi 1,257 na wa kuku 1,125 walitembelewa na kupewa ushauri juu ya ufugaji bora ili kuwa na mifugo imara na yenye afya. Huduma za chanjo kwa mifugo imezidi kuimarika ambapo zaidi ya ng'ombe 1,362 wamechanjwa ili kuwakinga na maradhi mbalimbali ikiwemo ugonjwa wa kimeta, chambavu na mapele ya ngozi. Aidha, jumla ya kuku 75,265 (Unguja kuku 66,120 na Pemba kuku 9,145) wamepatiwa chanjo dhidi ya maradhi

mbalimbali ikiwemo mahepe, gumboro, ndui (Fowl Pox) na "mareck's".

31. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuweka mikakati na mipango imara katika sekta hii ya kilimo ili kuiendeleza na kuwaendeleza wananchi wanaojihusisha nayo. Tumepanga kuimarisha huduma za matrekta katika mabonde yetu yenye ukubwa wa ekari 17,400 (Unguja 9,000 na Pemba 8,400) ili kuongeza uzalishaji hasa wa zao la mpunga; Tutaimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde yenye ukubwa wa hekta 370 na kuunga umeme wa njia kubwa bonde la Cheju B. Na kwa upande wa mifugo, Serikali imepanga kuongeza idadi ya wanyama watakaopata chanjo za maradhi ya miripuko kwa ng'ombe 30,000; kuku 200,000 na mbwa 8,000 pamoja na kupandishia ng'ombe 2,000 kwa njia ya sindano.

32. **Mheshimia Spika,** sekta ndogo ya misitu imeendelea kuvutia watalii wengi hasa wanaotembelea maeneo yetu ya hifadhi ikiwemo Msitu wa Jozani Unguja na Ngezi Pemba pamoja na mashamba ya viungo katika maeneo mbalimbali. Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imepanga kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu za misitu kutoka 16,085 hadi kufikia 100,000. Aidha, tumepanga kuongeza idadi ya miti kwa kupanda miti hekta 130 pamoja na kuihamasisha jamii kupanda hekta 300.

### Sekta ya Usafirishaji

33. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Usafirishaji inajumuisha usafiri wa baharini, usafiri wa nchi kavu na usafiri wa anga. Kwa upande wa usafiri wa baharini tayari Serikali imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkuu (Master Plan) wa Bandari ya Mangapwani uliojumuisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya eneo hilo. Mpango Mkuu huo umeainisha maeneo yatakayojengwa bandari mbali mbali pamoja na mahitaji mengine muhimu ikiwemo miundombinu ya barabara, umeme, maji safi na maji machafu. Kwa sasa

Wawekezaji kadhaa tayari wameshajitokeza kwa kuonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo. Serikali imekamilisha ujenzi wa Gati ndogo katika Bandari ya Mkokotoni ambayo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa maadhimisho ya Sherehe za Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kipindi kifupi imesajili meli za nje 85 zenye uzito wa GRT 641,351 katika usajili wa kimataifa baada ya kufunguliwa mwezi wa Septemba, 2021. Jumla ya Dola za Kimarekani 249,260 zimekusanywa kutokana na usajili huo tokea Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipoanza tena kusajili meli za nje. Vilevile, Serikali imeandaa utaratibu maalum wa kusajili vyombo vidogo vya baharini kwa lengo la kufuatilia usalama wake na hadi kufikia Machi 2022, jumla ya vyombo vidogo 788 vya baharini vimesajiliwa Unguja na Pemba.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali kupitia mpango wake wa Uimarishaji Viwanja vya Ndege imekamilisha ujenzi wa Ofisi za Watendaji katika Uwanja wa Ndege wa Nungwi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma. Aidha, katika kuimarisha huduma za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA), Serikali imeingia mkataba na Kampuni ya Kimataifa ya DNATA kwa ajili ya kutoa huduma katika uwanja huo kwa lengo la kuimarisha huduma na kuongeza mapato ya Serikali. Kampuni hiyo ya kimataifa, tayari imeshaleta vifaa mbali mbali vya kisasa vitakavyotumika kuhudumia ndege aina zote zinazowasili Zanzibar.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** usafiri wa nchi kavu ndio unaotumiwa na wananchi wengi hapa Zanzibar. Serikali tayari imeanza ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa kilomita 22.1 ambapo kazi hii inatarjiwa kukamilika ndani kipindi cha miaka miwili (2). Aidha, kwa upande wa miundombinu ya barabara za ndani, Serikali imekamilisha maandalizi ya

ujenzi wake zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba. Tayari hatua za kuzifanyia usanifu na michoro baadhi ya barabara zilizopendekezwa katika mradi huo zimeshaanza na barabara ya majaribio kutoka Kibonde Mzungu hadi Mwera yenye urefu wa kilomita 6.1 tayari imeshaanza kujengwa.

**Sekta ya Mawasiliano**

**37.** **Mheshimiwa Spika,** sekta ya mawasiliano ni sekta ya muungano na utekelezaji wake unafanywa kwa mashirikiano makubwa baina ya Wizara zetu zinazosimamia masuala ya mawasiliano. Hivi karibuni tulishuhudia zoezi la operesheni ya Anuani za Makaazi na Postikodi na kwa hapa Zanzibar linahusisha Shehia zote za Unguja na Pemba kwa kutoa namba za makaazi pamoja na kusajili taarifa za wakaazi katika Mfumo wa "National Physical Addressing (NaPA)" katika Shehia 59. Kazi hiyo inaendelea kwa Shehia zilizobakia Unguja na Pemba. Nawaomba sana viongozi na wananchi tutoe ushirikiano mkubwa katika kukamilisha zoezi hili.

**38.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinapatikana na kufikiwa katika maeneo yote ya mijini na vijjiini, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imetiliana saini na Kampuni ya Zantel kujenga minara 45 katika maeneo 42 Unguja na Pemba. Tayari Kampuni ya HTT Infraco limited imeshaanza ujenzi wa minara hiyo katika baadhi ya maeneo. Kukamilika kwa minara hii kutawezesha kuondoa changamoto ya mawasiliano katika maeneo mbali mbali mijini na vijijini.

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama**

**39.** **Mheshimiwa Spika,** maisha ya binaadamu pamoja na viumbe hai vyengine yanategemea sana maji. Hivyo suala la upatikanaji wa maji katika maeneo yetu ya mijini na mashamba linaendelea kuwa ni kipaumbele cha Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hali ya upatikanaji wa maji safi na salama hivi sasa imeanza kuimarika katika maeneo

mengi ya mijini ambapo hapo awali yalikuwa yanakabiliwa na ukosefu wa huduma hiyo. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imechukua hatua kubwa ya kuikarabati miundombinu ya maji pamoja na kuweka mifumo mipya sambamba kuuimarisha mfumo wa usambazaji maji uliokuwepo awali. ZAWA imefanya utanuzi na ukarabati wa mtandao wa maji kwa kulaza mabomba kwa eneo lenye ukubwa wa kilomita 8.3 (Unguja kilomita 5.6 na Pemba kilomita 2.7).

**40.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uzalishaji wa maji hivi sasa unakadiriwa ni wa wastani wa asilimia 55 kwa nchi nzima. Serikali imepanga kuongeza uzalishaji huo na kufikia wastani wa asilimia 75 kwa mwaka 2022/2023 kupitia Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar pamoja na miradi inayotokana na Fedha za IMF za UVIKO 19. Tayari utekelezaji wa mradi huo umeanza ambapo uchimbaji wa visima 35 kati ya visima 64 vinavyotarajiwa kuchimbwa umekamilika pamoja na ujenzi wa matangi ambao hadi sasa umefikia wastani wa asilimia 40. Sambamba na hili, kazi za ulazaji wa mabomba kwa mradi mzima imekamilika kwa wastani wa kilomita 64.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** wito wangu kwa wananchi ni kuendelea kutoa ushirikiano kwa wakandarasi wetu katika maeneo wanayotekeleza kazi zao ili hatimae kwa pamoja tuweze kufanikisha azma yetu ya kuondokana kabisa na tatizo la ukosefu wa maji safi na salama maeneo yote ya Unguja na Pemba. Na pia niendelee kusisitiza suala la utunzaji wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kutojenga karibu na vyanzo hivyo au kufanya shughuli zozote zitakazosababisha uharibifu wa miundombinu pamoja na maji yenyewe.

**Sekta ya Nishati**

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukua kila aina ya jitihada ili kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo yote wanapata huduma za nishati kulingana na mahitaji yao. Tayari Serikali imefanya mazungumzo na wawekezaji

mbali mbali juu ya kuwekeza katika sekta ya umeme hapa Zanzibar ambapo wawekezaji hao pia walipata fursa ya kuwasilisha taarifa juu ya uwezo wao wa kuwekeza katika Sekta hii.

43. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuweka mazingira rahisi ya wananchi kuunganishiwa umeme, idadi ya wananchi waliojitokeza kuomba na kuunganishiwa umeme Unguja na Pemba imeongezeka kufikia wateja wapya 19,823 na kuweza kupeleka umeme katika vijiji 36 (22 Unguja na 14 Pemba). Vilevile Serikali imezifanyia matengenezo laini kubwa za umeme zenye mkondo wa kilovolti 33 pamoja na kubadilisha nguzo mbovu 1,500 (nguzo 450 kwa Unguja na nguzo 1,050 kwa Pemba).

44. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imefanya matengenezo makubwa kwa kuondosha nyaya chakavu katika maeneo ya Kivunge hadi Nugwi (17.5km), Kitogani hadi Paje (11.5km) na Dunga hadi Ufufuma (6km) kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba Pandani hadi Masipa (1km), Pujini hadi Kichaka (15km) na Amani road hadi Ole (3km). Azma ya matengenezo hayo ni kuondoa kero za kukatika kwa umeme mara kwa mara pamoja na umeme kuwa mdogo. Kwa kiasi kikubwa Shirika limefanikiwa juu ya kuondosha kero hiyo kwa maeneo yaliyofanyiwa matengenezo.

45. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundo mbinu ya Umeme Zanzibar (CBMP) pia inaendelea na hatua za kupeleka umeme wa jua katika visiwa vya Kokota na Njau. Serikali itajenga vituo vya kupokea mionzi ya jua katika visiwa hivyo ambayo itabadilishwa na kuwa umeme wenye ukubwa wa kilowati 80 kwa kisiwa cha Kokota na kilowati 50 kwa kisiwa cha Njau.

46. **Mheshimiwa Spika,** nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo yote wanapata huduma za nishati

hii ya umeme kwa urahisi, uhakika na endelevu. Katika kufikia azma hiyo, tayari Serikali imesaini mkataba wa makubaliano kupitia Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (Zanzibar Energy Sector Transformation - ZEST). Bila shaka kukamilika kwa Mradi huu kutasaidia sana kuongeza idadi ya watumiaji wa umeme mijini na mashamba. Ni matumaini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa sote kwa pamoja tutaendelea kushirikiana katika kutunza miundombinu yetu ya umeme na kuendelea kuunga mkono jitihada zote zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha huduma hii muhimu.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa nishati za mafuta na gesi, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa upatikanaji wa nishati hiyo kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii unakuwa endelevu na kuepukana kabisa na tatizo la uhaba wa nishati hizo kila baada ya muda hasa mafuta. Miongoni mwa hatua hizo ni kubadilisha mfumo wa uingizaji wa mafuta wa kutumia Makampuni mengi (Multiple importers) na kuanzisha Mfumo wa Uingizaji Mafuta wa Pamoja (Bulk Procurement System – BPS) ambao unairuhusu Kampuni moja tu kuingiza mafuta kwa pamoja na kuyasambaza kwa wasambazaji wadogo wadogo hapa Zanzibar.

48. **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni kumekuwa na upandaji wa bei ya mafuta mfululizo hapa nchini hali ambayo inatokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Hali hii imeifanya Serikali kuchukua hatua kadhaa ili kupunguza ukali wa bei hiyo kwa wananchi ikiwemo kupunguza baadhi ya kodi za mafuta na baadhi ya tozo kwa bidhaa ya mafuta katika mwezi wa Disemba, 2021. Aidha, ZURA ililazimika kuhaulisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Ofisi - Pemba, ili zitumike katika kupunguza makali ya bei za mafuta.

49. **Mheshimiwa Spika,** uhalisia uliopo ni kuwa bei ya mafuta duniani bado inaendelea kupanda kutokana na

kinachoaminika kuwa ni vita inayoendelea baina ya Urusi na Ukraine. Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaendelea kutathmini namna bora ya kupunguza athari za mfumuko wa bei za mafuta katika masoko yetu ya ndani ili kuwapa nafuu wananchi wetu.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**50.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendeleza azma yake ya kuwafanya wananchi kuwa sehemu ya wazalishaji mali na watoa huduma kwa ajili ya kujipatia kipato wao binafsi na hatimae kuiongezea mapato Serikali. Serikali imeazimia kuwawezesha wananchi katika makundi mbalimbali ili waweze kuzalisha na kutoa huduma kibiashara na kupata tija zaidi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali tayari imeshaweka miongozo ya kisera na kisheria ya kusimamia suala hilo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** bila shaka uanzishwaji wa Wakala huyo kutapelekea uratibu mzuri zaidi na wa uhakika wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na masuala ya mafunzo na upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa wajasiriamalii na wafanyabiashara pamoja na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa wanazozalisha au huduma wanazotoa.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi vilevile limezingatiwa katika Programu zinazoendeshwa kutokana na fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya Uviko 19. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya CRDB imeanza kutoa mikopo nafuu kwa wananchi kwa ajili ya kuendeleza biashara na shughuli za ujasiriamali ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, jumla ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi 3,010,000,000 (Shilingi 1,107,500,000** Unguja na **Shilingi 1,902,500,000** kwa Pemba) imetolewa hadi Machi 31, 2022. Mikopo hiyo itaendelea kutolewa

kadri maombi yanavyopokelewa kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

53. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaamini kuwa shughuli za ujasiriamali na biashara kwa wananchi zina nafasi kubwa ya kujenga uchumi katika ngazi za kifamilia na taifa kwa jumla. Hivyo, Serikali imeandaa na kuweka mazingira na mifumo wezeshi ili kila mwananchi kwa kutumia kipaji na uwezo alio nao aweze kushiriki katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma bila kuvunja taratibu za kisheria zilizopo.

**Sekta ya Uwekezaji**

54. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwekezaji ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa uchumi wa nchi. Sekta hii inachochea kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta nyengine ikiwemo miundombinu, utalii na utoaji wa huduma. Kwa mnasaba huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua jitihada kubwa za kuweka mazingira yatakayovutia wawekezaji katika nyanja tofauti. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuweka mifumo mizuri ya kisera na kisheria na inayozingatia upatikanaji wa tija bila kuathiri mazingira, silka, mila na tamaduni zetu nzuri za Wazanzibari.

55. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeimarisha taratibu za upatikanaji wa vibali vinavyohusika na shughuli za uwekezaji kwa kuweka utaratibu wa 'One Stop Center". Kupitia utaratibu huu, muwekezaji anapatiwa huduma husika katika eneo moja na akikamilisha taratibu zote anaweza kupatiwa kibali cha ukaazi kwa siku moja. Mfumo huu umeanza kuleta mafanikio kwani katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, Serikali imesajili miradi ya uwekezaji 62 yenye mtaji wa takriban Dola za Kimarekani Milioni 449.08 na inatarajiwa kuzalisha ajira 4,479 kwa wananchi.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika kutafuta fursa zaidi za kutumia rasilimali zetu kwa maslahi ya nchi na watu wake, Serikali imevitangaza Visiwa Kumi (10) kwa ajili ya uwekezaji na tayari wameshajitokeza wawekezaji kwa visiwa hivyo. Jumla ya **Dola za Kimarekani Milioni 261.5** ni mtaji wa makisio unaotarajiwa kuwekezwa katika visiwa hivyo. Aidha, Serikali imeanza utaratibu wa kutangaza visiwa vyengine 10 kwa ajili ya uwekezaji ambapo visiwa 6 tayari wameshajitokeza wawekezaji na matarajio ni kukusanya malipo ya awali ya kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 5.8.**

57. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuongeza juhudi katika kuifanya sekta ya uwekezaji kuwa miongoni mwa sekta zitakazoongoza katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Tutaendelea kutanua zaidi fursa za uwekezaji kwenye visiwa; kuimarisha upatikanaji wa ardhi ya akiba; kuimarisha utoaji wa huduma kupitia kituo cha 'One Stop Center" na kutangaza fursa za uwekezaji ndani na nje ya nchi tukiamini kuwa bado kuna wawekezaji wengi hatujawafikia na wangehitaji kupata mazingira tuliyonayo ili kuendeleza biashara zao.

**Sekta ya Elimu**

58. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya elimu ina mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii yetu. Elimu bado iinaendelea kuwa ni msingi wa uhai na ukuaji wa sekta nyengine. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiipa kipaumbele kikubwa sekta hii kwa kuhakikisha kunakuwepo na mazingira bora ya kufundishia na kusomea katika maeneo yote. Ni jambo la kushukuru kuwa sekta hii ya elimu inaendelea kuimarika siku hadi siku ambapo kiwango cha uandikishaji wa watoto kimeongezeka sambamba na kuimarika kwa miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa na madawati.

59. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuweka mazingira bora ya kielimu ikiwemo kusambaza seti za madawati 11,342 (5,342 Unguja na 6,000

Pemba) ya wanafunzi katika Skuli za Sekondari Unguja na Pemba; kuufanyia marekebisho mfumo wa elimu kwa kurejesha darasa la saba katika ngazi ya elimu ya msingi kuanzia mwaka 2022, kuendelea kutekeleza mradi wa lishe ambapo jumla ya wanafunzi 14,437 wa Skuli 27 za Msingi zilizomo katika Mradi wa lishe wanaendelea kupatiwa chakula katika Wilaya saba za Unguja na Pemba. Sekta hii vilevile imefanikisha ukamilishaji wa madarasa 103 na kuzifanyia ukarabati skuli 36 pamoja na kukamilisha ujenzi wa vyoo 114 Unguja na Pemba.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya elimu inayotekelezwa kupitia fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya UVIKO 19, Serikali inaendelea na ujenzi wa skuli 9 za ghorofa katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba sambamba na ujenzi wa skuli mbili za Elimu Mjumuisho, ujenzi wa madarasa 805 yakiwemo mapya na ya kukamilishwa na ujenzi wa vyoo 1,693 pamoja na ukarabati wa skuli 24.

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali tayari imeanza ujenzi wa maabara katika skuli 10 za Sekondari zinazojengwa kwa lengo la kuimarisha elimu ya sayansi kwa wanafunzi wa sekondari Unguja na Pemba, kuwajengea uwezo walimu 303 wa skuli za msingi (darasa la 5 na 6) na walimu 939 wa sekondari (Kidato cha I na II) juu ya mbinu za ufundishaji masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza Unguja na Pemba. Mafunzo haya yatawasaidia walimu kumudu kufundisha vizuri masomo yao na kuweza kuinua zaidi kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia inachukua hatua ya kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo imeendelea kuwapatia aina 29 za vifaa visaidizi vikiwemo “braile”, miwani, “wheelchairs”, “white cane”, “telescope”, “special shoes”, “foot insole”, “foot orthosis” na “kitwalk”. Aidha, Progamu za lugha za alama zimerikodiwa katika Kituo cha Habari za Elimu – Kwarara kwa ushirikiano na wataalamu wa lugha ya alama kwa lengo la kuwasaidia

wanafunzi wenye mahitaji maalum ya ulemavu wa uziwi ili waendelee kupata fursa sawa ya kujifunza.

63. **Mheshimiwa Spika,** Serikali hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za kuanza rasmi utekelezaji wa Mradi wa Kuwajengea Uwezo Vijana ili waweze Kuajirika/Kujiajiri kupitia Elimu ya Amali na Uchumi wa Buluu (SEBEP). Mradi huu umekusudiwa kuimarisha miundombinu ya mafunzo ya amali kwa kujenga vyuo vitano vya mafunzo ya amali (vitatu Unguja na viwili Pemba) na kujenga Chuo cha Ubaharia katika eneo la SUZA Kampasi ya Nkurumah. Aidha, tutafanya utanuzi wa jengo la karakana ya makenika katika eneo la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na ujenzi wa "Incubator" katika eneo la Kizimbani kwa lengo kuwapatia fursa za kujiendeleza wajasiriamali wadogo wadogo.

64. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa kuwashukuru sana wananchi pamoja na Washirika wetu wa Maendeleo kwa mashirikiano na michango yao mikubwa katika kuendeleza elimu hapa nchini. Na pia natoa wito kwa wasimamizi wa masuala ya elimu kuendelea kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mipango na malengo ya Serikali katika utoaji wa huduma za elimu ili kuifikia azma tuliyojiwekea. Kwa upande wa jamii nayo naisihi kuendelea kushirikiana na Serikali katika kusimamia rasilimali za elimu pamoja na kuwahimiza watoto wetu juu ya umuhimu wa kusoma na kuwafuatilia kwa ukaribu zaidi katika mahudhurio na maendeleo yao ya kila siku. Serikali yetu imeweka mkazo zaidi katika kuinua ubora wa elimu Zanzibar.

**Sekta ya Afya**

65. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi, Serkali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuhakikisha kuwa huduma za kinga na tiba zinapatikana kwa makundi yote katika jamii. Kupitia Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Zanzibar imefanikiwa

kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi na wagonjwa wa Malaria. Kiwango cha ugonjwa huu kimendelea kuwa chini ya asilimia moja na wale wagonjwa wanaogunduliwa kuwa na Malaria hupatiwa matibabu stahiki pamoja na kufuatiliwa. Kushuka kwa kiwango cha maambukizi na wagonjwa wa Malaria kwa kiasi kikubwa kumetokana na hatua mbalimbali tulizozichukua ikiwemo upigaji dawa majumbani, usambazaji na utumiaji wa vyandarua pamoja na elimu za afya zinazotolewa na wataalamu wetu.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar pia ni moja ya nchi zilizopiga hatua katika udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI duniani. Hadi sasa Zanzibar inakisiwa kuwa na watu 7,647 wanaoishi na virusi vya UKIMWI ikiwa ni chini ya asilimia moja ya watu wote. Aidha, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa Zanzibar imefanikiwa kuvuka malengo ya dunia ya kufikia asilimia 90 tatu; ambapo asilimia 99.2 ya watu wanaoishi na VVU wanajijua hali zao, asilimia 98.6 ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI na asilimia 93 ya wanaotumia dawa za kupunguza makali ya virusi vimefubazwa kufikia chini ya kopi 1,000 kwa mililita ya damu.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba tarehe 18 Machi 2020 Zanzibar kiliripotiwa kisa cha mwanzo cha UVIKO – 19 na baadae jumla ya visa 2,554 na Vifo 79 vilivyosababishwa na janga hilo la UVIKO-19 viliripotiwa. Kutokana na hali ya ugonjwa huo, Serikali ilichukua juhudi mbalimbali pamoja na kuweka mikakati imara ya mapambano dhidi ya ugonjwa huu. Kwa vile bado visa hivi vinaendelea kuripotiwa maeneo mbalimbali duniani ni vyema wananchi wakaendelea kufuata maelekezo ya wataalamu wetu juu ya namna ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na kuwakinga wengine.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi yetu ya Utafiti wa Afya Zanzibar tayari imekamilisha utafiti wa kujua kinga katika miili ya wakaazi wa Zanzibar mara baada ya ugonjwa wa

Korona. Vile vile, taasisi inaendelea na utafiti wa ongezeko la thamani kwa dawa za miti shamba kwa kutibu maradhi yasiyoambukiza Zanzibar (value addition for herbal medicine used for managing non-communicable diseases in Zanzibar). Tunaamini matokeo ya tafiti hizi zitatumika katika kutatua matatizo ya kitabibu kwa magonjwa hayo yanayohusika.

69. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa huduma ya damu salama inaendelea kupatikana katika hospitali zetu za Unguja na Pemba ili kuwasaidia wagonjwa ambao wanahitaji huduma hiyo kwa haraka. Kwa kipindi cha Julai, 2021 - Machi, 2022 asilimia 72 ya unit za damu zilikusanywa kutoka kwa wachangiaji wa hiari na kuweza kusambazwa katika hospitali zetu. Tunawashukuru sana wananchi wote wanaochangia damu ambayo inasaidia katika kuokoa maisha ya wananchi wenzetu. Nawaomba waendelee na moyo huo na wote ambao hawakuchangia basi endepo itatokea fursa hiyo na ikiwa afya zao zinaruhusu kuchangia huduma hiyo tunawaomba wasisite kutoa mchango wao.

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za uchunguzi, tayari ujenzi wa jengo la maabara ya "Microbiology", "Phytochemistry" na maabara itakayotumika kupima virusi vya COVID -19 umekamilika. Aidha, taratibu za ujenzi wa maabara ya "Biochemistry" umeanza. Ni mategemeo yetu kuwa kukamilika kwa maabara hizi sambamba na upatikanaji wa vifaa muhimu kutarahisisha shughuli za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali pamoja na utibabu wa magonjwa hayo husika.

71. **Mheshimiwa Spika,** Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, imeendelea kutoa huduma za matibabu za kibingwa ikiwemo upasuaji wa uti wa mgongo na ubongo, usafishwaji damu kwa wagonjwa wa figo (dialysis), uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya saratani (chemotherapy), huduma za matibabu ya pua, koo na masikio.

**72. Mheshimiwa Spika,** katika mipango ya Serikali kwenye sekta hii ya afya ni pamoja na kuhakikisha huduma za tiba za kibingwa zinapatikana kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa; kuanzisha huduma maalum za afya kwa watalii (Medical Tourism) ambapo miundombinu ya afya itaboreshwa na kujenga hospitali za kisasa zitakazokuwa na uwezo wa kuhudumia watalii nchini; kuanzisha na kuimarisha kambi za matibabu kwa kutumia madaktari kutoka nje ili kupunguza kusafirisha wagonjwa wetu kwenda nje ya Zanzibar kwa matibabu; na kujenga hospitali mpya ya wagonjwa wenye matatizo ya akili eneo la Kinyasini Pemba na hospitali ya mkoa wa kaskazini Unguja eneo la Mahonda.

**73. Mheshimiwa Spika,** sekta ya afya pia imebahatika kufaidika na fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya UVIKO 19 na inandelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye mnasaba na maendeleo ya huduma za afya. Miongoni mwa miradi hiyo ni ununuzi wa majokofu manne ya kuhifadhia damu, vifaa vya kukusanyia damu, "platelets agitators" na "blood sealers"; ujenzi wa hospitali 10 za wilaya na hospitali moja (1) ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Lengo la ujenzi wa hospitali hizi ni kuipunguzia mzigo Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

**Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia na Udhalilishaji**

**74. Mheshimiwa Spika,** Serikali yetu bado inachukizwa sana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia ambavyo vimekuwa vikiripotiwa mara kwa mara katika jamii zetu. Takwimu rasmi za Ofisi ya Mtakwmu Mkuu wa Serikali zinaonyesha kwamba bado idadi ya matukio haya inaongezeka siku hadi siku na kupelekea ongezeko kubwa la waathirika. Kwa mwaka 2021 takwimu rasmi zinaonyesha kuwa jumla ya matukio 1,222 ya udhalilishaji wa wanawake na watoto yameripotiwa ambapo idadi ya watoto ni 1,068 sawa na asilimia 87.4 na wanawake ni 154 sawa na asilimia 12.6.

75. **Mheshimiwa Spika,** takwimu hizo zinaonyesha jinsi hali halisi ya suala hili la udhalilishaji ilivyo mbaya hadi sasa katika nchi yetu. Kwa mwaka 2021 kwa Wilaya yenye idadi kubwa ya matukio haya ni Wilaya ya Mjini, ikifuatiwa na Magharibi 'B' na Magharibi 'A'. Kwa mwaka 2022, taarifa zilizopokelewa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ni za mwezi wa Januari na Februari. Kwa mwezi wa Januari jumla ya matukio 65 yaliripotiwa ambapo watoto ni 49 sawa na asilimia 75.4 na wanawake ni 16 sawa na asilimia 24.6). Kwa upande wa mwezi wa Februari matukio hayo yameongezeka hadi kufikia 100 (watoto 84 sawa na asilimia 84 na wanawake 16 sawa na asilimia 16) ambapo matukio mengi yaliripotiwa Wilaya ya Wete (matukio 23) ikifuatiwa na Magharibi 'B' (17) na Magharibi 'A' (14).

76. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Serikali yetu inaendelea kuchukua jitihada zaidi katika kupiga vita na kulimaliza tatizo hili kupitia maeneo matatu (3) makuu ya utekelezaji. Eneo la kwanza ni Kinga; katika eneo hili juhudi zilizotekelezwa ni pamoja na kuunda na kuziimairisha Timu za Viongozi wa Dini za Wilaya za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutoa taarifa ya matukio na kuchukua hatua dhidi ya sababu zinazochangia vitendo hivyo katika maeneo yao, kuendesha Programu maalumu ya uelimishaji na uhamasishaji wanafunzi na walimu katika skuli za msingi na Sekondari, kuelimisha jamii kupitia vyombo vya Habari jinsi ya kujikinga na kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kuanzisha na kuendeleza Mabaraza ya Watoto katika Ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa katika kukabiliana na tatizo la vitendo vya udhalilishaji.

77. **Mheshimiwa Spika,** eneo la pili ni kuweka mazingira wezeshi ya kisera, sheria, uratibu na takwimu. Katika eneo hili Serikali inafanya marekebisho na kupitishwa kwa Sheria mpya zikiwemo Mahakama ya Kadhi ya mwaka 2017, Makosa ya Jinai 2018, Ushahidi 2016, na Mwenendo wa Makosa ya Jinai 2018, kuanzishwa kwa Mahakama

za Watoto na Mahakama maalum ya kushughulikia kesi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji, kuanzishwa na kufanyiwa kazi mfumo wa uratibu kuanzia ngazi ya Shehia hadi Taifa pamoja na kuanzishwa na kufanya kazi kwa mfumo wa Takwimu za vitendo vya ukatili na udhalilishaji ambao unasimamiwa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Mfumo huu unakusanya na kutoa taarifa za kila mwezi na kusambazwa kwa wadau kupitia vyombo vya habari.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** eneo la tatu ni utoaji wa huduma bora za ushughulikiaji na usaidizi. Katika eneo hili mambo muhimu yanayofanyika ni pamoja na kutengeneza na kuimarisha miongozo ya utoaji wa huduma mbali mbali kwa waathirika wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji, kuandaa na kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii ikiwemo huduma ya ushauri nasaha kwa waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, kuanzisha na kutoa huduma ya nyumba salama kwa waathirika wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanaohitaji na kuanzisha vikundi maalum vya Wilaya vya wasaidizi wa Sheria kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa waathirika wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji pamoja na elimu ya sheria kwa jamii.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuweka mipango na mikakati zaidi pamoja na kusimamia utekelezaji wake dhidi ya vitendo hivi ili kuweza kuvitokomeza kabisa. Aidha, tutaendeleza mashirikiano na wadau wa ndani na nje katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuimarisha mapambano haya. Nitoe wito kwa jamii kuwa kila mmoja wetu ana jukumu la kuilinda jamii yetu ili kuepukana na vitendo hivi viovu vya udhalilishaji. Vilevile, sote kwa pamoja tuendelee kuwa tayari kutoa kila aina ya msaada unaohitajika katika mapambano haya. Kwa pamoja tutashinda katika kutokomeza kadhia hii.

80. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi juu ya hali ya shughuli mbalimbali za Serikali za baadhi ya sekta, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na malengo yake ya mwaka 2022/2023.

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2021/2022

81. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, zinatekelezwa kupitia Idara saba, Taasisi tatu pamoja na Vitengo sita vinavyoripoti moja kwa moja kwa Katibu Mkuu. Kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutekeleza majukumu yake kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Programme Based Budget), Ofisi kupitia Idara na Taasisi hizo inatekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14.

## OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (C01)

**PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

***Programu Ndogo (SC010101) : Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais***

82. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais ambayo jukumu lake ni kuratibu kazi za kila siku pamoja na utoaji wa huduma zote muhimu kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeratibu ziara 60 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ndani ya nchi (Unguja, Pemba na Tanzania Bara) (Kiambatisho Nam. 1).

ii. Imeratibu na kuendesha vikao 11 baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Mabalozi pamoja na Wageni mashuhuri kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na mahusiano ya Kitaifa na Kimataifa.

iii. Imeratibu na imefuatilia utekelezaji wa ahadi alizozitoa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar zinazolenga kuleta maendeleo katika upatikanaji wa huduma za jamii. Jumla ya ahadi 11 zimetolewa na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais katika maeneo mbalimbali wakati alipokuwa anafanya ziara za kikazi.

iv. Ofisi imeratibu utatuzi wa malalamiko, migogoro na kero mbalimbali za wananchi ambapo jumla ya Malalamiko/ Migogoro 174 imepokelewa kati ya hayo malalamiko 13 tayari yamepatitiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na Taasisi husika. Aidha, Ofisi inaendelea kufuatilia kwa ukaribu hatua zinazochukuliwa katika kuyapatia ufumbuzi malalamiko yaliyobaki katika Taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi.

v. Ofisi imeendelea kuweka kumbukumbu za matukio ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar zikiwemo hotuba 34 na Picha 925 za matukio mbalimbali aliyoshiriki.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Programu yake Ndogo iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,825,256,455** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 820,516,570** ambazo ni sawa na **asilimia 56** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 45** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka .

## PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuweka mfumo imara na endelevu wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa jamii kupitia Programu Ndogo nne (4) ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za SMZ Dodoma.

### Programu Ndogo (SC010101) : Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa hapa Zanzibar. Katika kipindi cha miezi tisa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imeratibu utoaji wa huduma za uokozi na upatikanaji wa misaada ya kibinaadamu katika matukio 79 ya majanga yaliyotokea Unguja na Pemba. Kati ya hayo matukio ya moto 64; ajali za baharini 5 zilizopelekea watu 11 kupoteza maisha na watu 11 kuokolewa wakiwa hai na matukio 7 ya upepo mkali yaliyopelekea kuezuka mapaa nyumba 200 (194 Unguja na 6 Pemba).

ii. Vilevile, Ofisi imeratibu upatikanaji wa huduma za kibinaadamu kwa familia zilizofikwa na misiba miwili (2) iliyotokana na vifo vya watu 13 (9 Pemba na 4 Unguja) baada ya kula nyama ya kasa katika eneo la Taponi Shehia ya Msuka Magharibi na maeneo jirani Pemba pamoja na Shehia ya Matemwe Mbuyu Maji Unguja. Aidha, jumla ya watu 88 wameathirika kiafya na tukio hilo la kula nyama ya kasa (48 Pemba 40 Unguja).

iii. Ofisi imetoa tahadhari kwa wadau wote wa kukabiliana na maafa juu ya muelekeo wa mvua za vuli za mwaka 2021 pamoja na kufanya kikao kimoja na wadau juu ya kuweka mikakati inayopaswa kuchukuliwa ya tahadhari za mapema kutokana na muelekeo wa mvua hizo. Tahadhari hizo zilisaidia kwa kiasi kikubwa ambapo athari za mvua hizo zilionekana kupungua. Sambamba na hilo, Ofisi imeendelea kutoa tahadhari za muelekeo wa mvua za Masika za mwaka 2022 kwa kutoa matangazo kupitia ZBC redio na televisheni, kutuma ujumbe mfupi wa pamoja (bulk sms) na kutoa tahadhari hizo kwa wenyeviti wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Shehia.

iv. Ofisi imetoa elimu ya kujikinga na kukabiliana na matukio ya majanga katika skuli za Unguja na Pemba ambapo jumla ya wanafunzi 2,487 wamepatiwa elimu hiyo, kati ya hao wanafunzi 52 kutoka Skuli ya Sekondari ya Ali Hassan Mwinyi, wanafunzi 35 kutoka Skuli ya Mtopepo pamoja na wanafunzi 2,400 kutoka Skuli 14 za Dakhalia/Kambi zilizopo kisiwani Pemba zikiwemo Skuli za Ambasha Islamic, Wete Islamic, Amini Islamic, Laurent, Farahedy, Moh'd Juma Pindua, Madungu Sekondari, Shamiani, Fidel Castro, Chuo cha Kiislamu Kiuyu, Ali Khamis Camp, Chasasa Sekondari, Utaani na Kengeja – Ufundi.

v. Vilevile, elimu hiyo pia imetolewa kwa Wenyeviti wa Kamati zote 389 za Kukabiliana na Maafa za Shehia Unguja na Pemba, wajumbe wa kamati ya uvuvi ya Jambiani pamoja na vijana 68 wa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya ya Mjini, Kati, Kaskazini "A" na Kaskazini "B". Pia, elimu imetolewa kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi 6 vimerushwa hewani kupitia Televisheni ya Shirika la Utangazaji Zanzibar na Zanzibar Cable TV.

vi. Ofisi imefanya vikao viwili vya Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa mwezi Septemba, 2021 kwa lengo la kujadili hali halisi ya mwenendo wa UVIKO-19 pamoja na kuwasilisha taarifa ya mapitio ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2021.

vii. Vilevile, Ofisi imetoa vifaa vya mawasiliano ya dharura (redio calls) kwa wadau wake wakiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Hali ya Hewa, Kituo cha Mawasiliano ya Dharura pamoja na Wizara ya Afya kwa lengo la kuunganisha mawasiliano ya dharura.

viii. Ofisi imefanya matengezo ya mitambo ya mawasiliano iliyopo Micheweni Pemba pamoja na kufanya ukaguzi katika vituo vya mawasiliano vilivyopo Gamba, Makunduchi na Maruhubi pamoja na eneo la minara Masingini ili kuhakikisha kwamba mitambo hiyo inafanya kazi iliyokusudiwa.

ix. Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Red Cross Tanzania na Red Cross ya Uingereza imeratibu zoezi la mradi wa kuwasaidia wananchi walioathiriwa na UVIKO-19 ambapo jumla ya Shilingi 48,000,000 zilitumika. Zoezi hilo limefanywa kwa majaribio hapa Zanzibar katika Wilaya za Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Kati ambapo jumla ya wananchi 300 wamefaidika kwa kila familia moja imepatiwa Shilingi 85,000 kwa awamu mbili.

x. Ofisi imeandaa rasimu ya Kanuni za Mfuko wa Maafa na Kanuni za Kukabiliana na Maafa za mwaka 2021.

xi. Ofisi imeratibu uzinduzi wa vijiji vya wananchi walioathiriwa na mvua za Masika za mwaka 2017 vilivyopo Nungwi (Unguja) na Tumbe (Pemba). Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 23 Novemba 2021 huko Nungwi Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja ambapo jumla ya familia 57 (27 Nungwi na 30 Tumbe) zinaishi katika nyumba hizo.

xii. Ofisi imeandaa muongozo utakaotumika kwa ajili ya uendeshaji wa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kilichopo Maruhubi Unguja.

xiii. Ofisi imeandaa mfumo wa kutunza takwimu za matukio ya majanga na maafa yanayotokea ambapo hatua inayofuata ni kuuweka Mfumo huo katika Mifumo ya wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuanza kazi na kutumika.

xiv. Ofisi imekamilisha uandaaji wa toleo la pili la Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2021.

xv. Ofisi imewajengea uwezo Wenyeviti na Kamati za Kukabiliana na Maafa za Shehia zote Unguja na Pemba juu Ukusanyaji, Uhifadhi na Uwasilsihaji wa Takwimu za matukio ya majanga na maafa yanayotokea katika maeneo yao kupitia dodoso maalum la kukusanyia takwimu lililoandaliwa.

xvi. Ofisi imeratibu vikao viwili (2) vya robo mwaka kwa Kikosi kazi cha kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kutokomeza Kipindupindu Zanzibar wa mwaka 2018 – 2027.

**86.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamisheni iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,387,000,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 635,718,259** ambazo ni sawa na **asilimia 50** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 46** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka .

**Programu Ndogo – SCO10202: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa**

**87.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika kipindi

cha miezi tisa (Julai 2021 – Machi 2022) imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imeratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kilele chake kilifanyika Uwanja wa Amaan tarehe 12 Januari 2022.

ii. Ofisi imeratibu ushiriki wa wananchi na Viongozi wa Zanzibar katika kilele cha Sherehe za Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika tarehe 9 Disemba 2021 katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam.

iii. Ofisi imeshiriki katika vikao vya maandalizi ya Sherehe za Miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambapo kilele chake kimefanyika kwa uzinduzi wa Kitabu cha Historia ya Muungano pamoja na Kongamano lenye mnasaba wa shughuli hiyo. Shughuli hii imefanyika Dodoma tarehe 26 Aprili 2022.

iv. Ofisi imefanya matayarisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi pamoja na Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume.

v. Ofisi imefanya ziara pamoja na matengenezo ya makaburi ya Viongozi wa Kitaifa; makaburi yaliyofanyiwa matengenezo ni Kaburi la Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, Marehem Sheikh Idriss Abdul-Wakil na Marehemu Sheikh Thabit Kombo Jecha ikiwa ni utaratibu wa kuyatunza makaburi hayo.

vi. Ofisi imeendelea kukusanyanya mapato yanayotokana na huduma za ukodishaji wa maduka yaliyopo Mwanakwerekwe pamoja na kukodisha vifaa vya sherehe.

**88.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,243,681,493** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 874,318,862** ambazo ni sawa na **asilimia 74** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 70** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 49,422,000** ikiwa ni mapato yatokanayo na ukodishaji wa maduka na vifaa vya Sherehe, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022 Idara imekusanya jumla ya **Shilingi 22,065,000** ambayo ni sawa na **asilimia 55** kwa fedha iliyotengwa miezi tisa na **asilimia 45** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**Programu Ndogo – SCO10203: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** Program Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, masuala ya Muungano, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo ambayo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2021 – Machi 2022), imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imeratibu utoaji wa vibali 405 kwa watafiti wa ndani na nje ya Nchi ikijumuisha Taasisi 32 (Serikali 13 na binafsi 19), wageni 22 na wenyeji 351.

ii. Ofisi imeandaa taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 kwa utekelezaji wa kipindi cha mwaka mmoja ambayo imeelezea hali halisi ya utekelezaji katika sekta za Serikali za kijamii na kiuchumi.

iii. Ofisi imeratibu na kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kuendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho ya Sheria namba 4 ya mwaka 2012 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria.

iv. Ofisi imeratibu na kusimamia uingizaji wa fedha kwa majimbo yote 50 ya Uwakilishi ya Unguja na Pemba ambapo hadi kufikia Machi Majimbo 29 tayari yameingiziwa fedha hizo.

a) Ofisi imefanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Wawakilishi katika majimbo yote ya Unguja na Pemba. Aidha, imeratibu na kushiriki katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya Wabunge katika Manispaa/Baraza la Mji/Halmashauri zote za Unguja na Pemba pamoja na kutoa mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha (financial statement) yalitolewa tarehe 02/03/2022.

v. Ofisi imefuatilia Mkutano wa nne, watano na wasita wa Baraza la Kumi la Wawakilishi pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Baraza na ahadi zilizotolewa na Mawaziri katika Mikutano hiyo.

vi. Ofisi imeandaa na imeshiriki vikao vitatu vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kuhusu Masuala ya Muungano. Vikao hivyo, vilifanyika Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar ambavyo pamoja na mambo mengine vilifanya maandalizi ya Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara (ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri), Kikao cha Makatibu Wakuu, Kikao cha Mawaziri na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Aidha, Sekretarieti iliandaa Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ kinachotarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2022.

vii. Ofisi iliandaa Kikao cha Kamati ya Fedha, Biashara na Uchumi kwa ngazi ya Makatibu na Wakuu Mawaziri kilifanyika tarehe 2 – 3 Agosti, 2021; Kikao cha Makatibu

Wakuu wa SMT na SMZ kilichofanyika tarehe 10 Agosti, 2021; Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ kilichofanyika tarehe 23 Agosti, 2021. Vikao hivi Makatibu Wakuu na Mawaziri pamoja na mambo mengine vilipendekeza kuondolewa Hoja 11 miongoni mwa hoja za Muungano katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kinachofuata.

viii. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliratibu, kuandaa na kushiriki kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kilichofanyika Zanzibar tarehe 24 Agosti, 2021 ambacho pamoja na mambo mengine kiliridhia kuondolewa kwa hoja 11 na kusainiwa kwa Hati tisa (9) za kuondoa Hoja/ Changamoto za Muungano **(Kiambatisho Nam. 2).**

ix. Ofisi imeshiriki katika vikao 17 vya ushirikiano baina ya Wizara za SMZ na SMT vilivyofanyika katika Zanzibar na Tanzania Bara **(Kiambatisho Nam. 3).** Pamoja na mambo mengine, vikao hivyo vimeweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta zao.

x. Ofisi imeratibu na kushiriki katika uandaaji wa andiko la "Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar" ambalo linatarajiwa kuwa ni rejea muhimu kwa wananchi kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

xi. Ofisi imeratibu na kusimamia ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaomiliki maeneo ya jirani na eneo la Ofisi na Makaazi ya Makamu wa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Red Zone), lililopo Tunguu. Jumla ya **Shilingi 2,235,081,850** zimetumika kuwalipa wananchi na tayari wameshakabidhi maeneo yao pamoja na mali zilizomo. Fedha hizo zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

xii. Ofisi imetayarisha na kurusha hewani kipindi Maalumu cha Mafanikio ya mwaka mmoja wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (Redio) tarehe 19 Machi, 2022 pamoja na kutoa elimu kwa Umma juu ya Utatuzi wa Hoja 11 zilizoondolewa katika orodha ya hoja za Muungano.

xiii. Ofisi imeandaa Muongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera za Sekta za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakaotumiwa na Wizara katika uandaaji wa Sera zao.

xiv. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, Ofisi imesimamia na kuratibu Uhaulishaji Fedha kwa Kaya za Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (Conditional Cash Transfer) ambao umewaongezea kipato Walengwa wa Mpango na kuweza kumudu mahitaji ya msingi ya kimaisha ikiwemo uhakika wa upatikanaji wa chakula pamoja na upatikanaji wa huduma za afya na elimu kwa watoto wa kaya 30,692 (Unguja kaya 16,992 na Pemba kaya 13,700) ambazo zimelipwa ruzuku zao kwa vipindi vinne (4) vya malipo ikiwa ni Shilingi 5,735,692,496.00 (Unguja Shs. 2,914,283,691.00 na Pemba 2,821,408,805.00).

xv. Aidha, Ofisi imesimamia na kuratibu Utekelezaji wa Miradi 184 (Unguja 110 na Pemba 74) ya kutoa Ajira za Muda (Public Works Program – PWP) kwa Kaya za Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambapo Shilingi 890,185,000.00 (Unguja 495,157,000.00 na Pemba 395,028,000.00) zimetumika. Pia, Shilingi 966,228,000.00 zililipwa kwa Walengwa kati ya hizo (Unguja 363,120,000.00 na Pemba 603,108,000.00) zikijumuisha kaya 23,200 kati ya hizo (Unguja 12,863 na Pemba 10,337) ukiwa ni ujira wa ushiriki wao wa kazi kwa kipindi cha kwanza cha kazi na Walengwa hao wameweza kuongeza kipato cha kaya; kupata ujuzi kwa kaya shiriki na kutengeneza mali ya jamii katika sekta za Misitu, Maji, Kilimo cha Umwagiliaji, Uvuvi, Mazingira, barabara/usafirishaji na sekta ya Elimu kupitia ukarabati wa madarasa na majengo mengine ya elimu.

xvi. Vilevile, Ofisi kupitia mradi wa TASAF imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi mitatu (3) ya Miundombinu/ Ujenzi ikiwemo: Ujenzi wa Ukumbi wa Mitihani katika Skuli ya Kizimkazi Dimbani ambao umefikia asilimia 90 hadi kufikia mwezi Machi, 2022 na kugharimu Shilingi 133,731,121.66; Ujenzi wa Kituo cha Afya Shehia ya Kendwa ambao hadi kufikia Machi umegharimu Shilingi 119,416,000.00; na ukarabati wa madarasa 10 na ujenzi wa ukuta katika Skuli ya Piki ambapo jumla ya Shilingi 37,854,000.00 zimetumika.

xvii. Kwa upande wa kuwekeza kwa ajili ya kukuza uchumi wa Kaya Ofisi imeratibu na kuwawezesha kujiwekea akiba na kuwekeza katika vikundi pamoja na kumwezesha mwanakaya kuwa na mpango endelevu wa kuondokana na umasikini kwa kujitegemea. Aidha, Ofisi imewapatia wana kaya hao ujuzi na fursa za kilimo na biashara ambapo vikundi 1,147 kwa Unguja vyenye jumla ya kaya 16,009 (wanawake 15,395 na wanaume 614). Pia, kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, ofisi imeanza utaratibu wa kuvisajili rasmi vikundi vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ili viweze kufikia malengo ya kujiendesha kibiashara pamoja na kuzifikia fursa stahiki zinazotolewa na Serikali.

xviii. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwawezesha walengwa katika kujiwekea akiba na kuwekeza, TASAF kupitia Shirika la CSR iliendesha zoezi la majaribio la kuweka akiba na kuwekeza kwa kaya 629 kati ya kaya 640 (98%) katika Shehia 16 zinazotekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini.

xix. Vilevile, Ofisi imeratibu Kikao cha Kamati ya Usimamizi (Steering Committee) - TASAF Unguja ambacho pamoja na mambo mengine kilipitisha na kuidhinisha miradi ya vituo vya afya katika Shehia za Uzi na Upenja. Aidha, Ofisi imeratibu ziara ya ufuatiliaji na kujifunza kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyofanyika tarehe 12 hadi 13 Februari, 2022. Kupitia ziara hiyo Waheshimiwa Wajumbe walipokea Taarifa ya

Utekelezaji wa Mpango pamoja na kutembelea miradi katika Shehia za Fujoni, Mahonda, Mkataleni na Kizimkazi Dimbani. Vilevile, tarehe 06 – 10/03/2022 imeratibu na kusimamia ziara ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mkoani Njombe ambapo Kamati ilitembelea Miradi ya TASAF inayofadhiliwa na nchi zinazozalisha mafuta duniani kwa wingi (OPEC).

xx. **Mheshimiwa Spika,** Pia, Ofisi imeendesha mafunzo rejea kwa Maafisa 14 wa Afya na Elimu wa Wilaya kwa lengo la kuhakikisha fomu za masharti ya elimu na afya kwa kaya za walengwa zinajazwa kwa usahihi na haraka ili kulifikia lengo la ruzuku za masharti ya elimu na afya.

**91.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 689,096,781** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 368,578,145** ambazo ni sawa na **asilimia 73** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 53** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka .

Aidha, Programu hii Ndogo kupitia Programu ya TASAF ilipanga kutumia **Shilingi 37,722,600,000** kwa kazi za maendeleo ambapo **Shilingi 37,622,600,000** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2022 ilipata jumla ya **Shilingi 8,556,988,252** (23%) ambapo **Shilingi 8,481,988,252** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo sawa na **asilimia 27** na **Shilingi 75,000,000** ni mchango wa Serikali sawa na **asilimia 75.**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Baraza hili liliidhinisha matumizi ya **Shilingi 16,118,600,000** ikiwa ni ruzuku kwa Idara ya Uhamiaji, Zanzibar na hadi Machi 2021 ilipata **Shilingi 4,200,000,000** ambazo ni sawa na **asilimia 35** kwa fedha zilizotengwa miezi tisa na **asilimia 26** kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka.

**Programu Ndogo – SCO10204: Shughuli za SMZ Dodoma**

**93. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ Dodoma jukumu lake kuu ni kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara yenye lengo la kukuza na kuimarisha ushirikiano baina SMZ na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kimataifa na Ofisi za Kibalozi na Asasi nyengine. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imeratibu na kushiriki vikao katika wizara za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma, Wizara hizo ni Wizara ya Ardhi nyumba na Makaazi, Wizara ya Muungano na mazingira, Ofisi ya Waziri mkuu, Bunge na Sera, Waziri wa Fedha na Mipango na Wizara ya Ulinzi. Lengo ni kujenga mahusiano ya karibu kati ya SMZ na SMT. Pamoja na mambo mengine Wizara ya Ardhi waliahidi upatikanaji wa Viwanja kwa watendaji wa SMZ.

ii. Ofisi imeratibu upatikanaji wa huduma ya usafiri wanapokuwa Tanzania Bara pamoja na upatikanaji wa VISA kwa Viongozi na watendaji wa SMZ.

iii. Ofisi imeendelea kuitangaza Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma kwa niaba ya Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushiriki Tamasha la Biashara la sabasaba. Tamasha hilo limesaidia kutambulika kwa Ofisi na kuongeza mashirikiano ya karibu baina ya Wizara na Taasisi na SMZ na Wizara na Taasisi za SMT. Aidha, Ofisi imeratibu na kushiriki kipindi kimoja (1) katika Shirika la Utangazaji Zanzibar juu ya Uwepo wa Ofisi ya Uratibu Sgughuli za SMZ Dodoma pamoja na majukumu yake.

iv. Ofisi imeratibu na kushiriki vikao 50 vya mashirikiano ya kazi baina ya Wizara za SMZ, SMT, Ofisi za Kibalozi, Taasisi na Jumuiya za Kimataifa. Kupitia vikao hivyo pande zote zinazohusika zimeainisha maeneo ya mashirikiano ili kuleta

tija katika sekta za kiuchumi, kijamii na kisiasa ikiwemo fursa za uwekezaji, uanzishwaji wa miradi ya maendeleo na kuinua sekta ya Utalii **(Kiambatisho Nam. 4).**

**94.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali-Dodoma iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 671,107,912** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 361,397,289** ambazo ni sawa na **asilimia 70** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 54** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka .

**PROGRAMU KUU - (PCO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inahusika na uimarishaji wa mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za kiofisi. Programu hii ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba.

**Programu Ndogo – CO10401: Uongozi na Utawala**

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na inahusika na usimamizi wa rasilimali watu na utekelezaji wa kazi za kila siku za Ofisi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo za mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), pamoja na stahiki nyenginezo. Aidha, wafanyakazi 17 wamerekebishiwa mishahara yao baada ya kurejea masomoni.

ii. Idara imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 41 wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi. **(Kiambatisho Nam. 5).** Vile vile, wafanyakazi 22 wamepatiwa mafunzo ya awali (induction course) katika Chuo cha Utawala wa Umma, Zanzibar.

iii. Wafanyakazi 32 wamepandishwa madaraja kwa mujibu wa muundo wa utumishi Serikalini **(Kiambatisho Nam. 6).**

iv. Ofisi imekamilisha kazi za uimarishaji wa Mifumo ya Mawasiliano ambayo inahusisha:

   a) Government portal: www. zanzibar.go.tz, Tovuti ya Ofisi: www. Ompr.go.tz, Jarida la Makamu Toleo la Kwanza litakalochapishwa Mara 4 kwa mwaka.

   b) Mfumo wa uwekaji wa taarifa za Watumishi kwa njia ya Kielektroniki (Kanzidata).

v. Ofisi imeimarisha Mfumo wa ulinzi wa Ofisi na Upekuzi (CCTV Camera na Scanner Metal Detector).

vi. Ofisi Imetoa huduma za mikutano 93 katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil. Kati ya mikutano hiyo, 8 ilihudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; Mkutano 1 ulihudhuriwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman; Mikutano 7 ilihudhuriwa na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla; na mikutano 77 ilihudhuriwa na viongozi waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

vii. Ofisi imefanya ukarabati wa majengo yote yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**97.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,571,839,909** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia

Machi, 2022 imetumia **Shilingi 852,250,923** ambazo ni sawa na **asilimia 71** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 54** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka .

***Programu Ndogo – CO10402: Mipango, Sera na Utafiti***

**98. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na uratibu wa masuala ya bajeti, uibuaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, masuala ya sera na tafiti zinazohusu masuala yanayosimamiwa na Ofisi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeandaa Mpango kazi na Mpango wa Utekelezaji wa mwaka 2021/2022, Taarifa ya utekelezaji wa Robo ya kwanza, Nusu Mwaka na Taarifa ya Utekelezaji ya Miezi Tisa 2021/2022 pamoja na kuandaa bajeti ya mwaka 2022/2023.

ii. Ofisi imefanya ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa miradi na shughuli zinazosimamiwa na Ofisi pamoja na kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini za mwezi, robo mwaka na miezi tisa kwa mwaka 2021/2022 na kuziwasilisha sehemu husika;

iii. Ofisi imetoa mafunzo kwa maafisa Takwimu/Mipango juu ya uandaaji wa viashiria na nyenzo za kukusanyia taarifa za takwimu za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

iv. Ofisi imetoa mafunzo ya Uandaaji wa Bajeti kwa Maafisa Mipango wa Idara/Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuwajengea uwezo na uelewa wa pamoja katika masuala yanayohusiana na maandalizi ya bajeti.

v. Ofisi imeanza hatua za awali za kuandaa Mpango Mkakati wa Takwimu wa Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

vi. Afisi imezipitia Sheria mbili na Kutengeneza Kanuni mbili ambazo ziko katika hatua tofauti. Sheria hizo ni Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), 2021 ambayo tayari imewasilishwa Baraza la Mapinduzi na Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo iliyopo Tume ya Kurekebisha Sheria. Aidha, Kanuni zilizotengenezwa ni Kanuni za Bendera ya Zanzibar, Nembo , Wimbo wa Taifa na Wimbo Maalum za 2021 ambayo imewasilishwa Baraza la Mapinduzi na Kanuni ya Kukabiliana na Maafa ambayo ipo katika hatua ya kupokea maoni ya wadau;

vii. Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM) ambapo ziara za utekelezaji katika maeneo ya miradi kwa Unguja na Pemba zimefanyika. Lengo ni kubaini mafanikio na changamoto katika maeneo hayo na kuwapatia ushauri wa kitaalamu watekelezaji wa Miradi hiyo. Aidha, Kitengo kimeendesha vikao vitatu vya Kamati Tendaji na kufanya uchaguzi wa majimbo sita ya ZGFCCM.

**99. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 450,331,485** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 199,372,312** ambazo ni sawa na **asilimia 59** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 44** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

***Programu Ndogo – CO10403: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi - Pemba***

**100. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba. Kwa vile shughuli zinazofanywa na Idara na Taasisi za Ofisi Unguja vilevile hutekelezwa Pemba, Programu hii inahusika zaidi na uratibu wa shughuli hizo kwa Pemba sambamba na shughuli za kiutawala za kila siku. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2021/2022. Programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imeratibu ziara nne (4) za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais - Pemba;

ii. Ofisi imeandaa mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

iii. Ofisi imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pemba kwa Program na Miradi ya Maendeleo ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

iv. Aidha, Ofisi imeratibu shughuli za Serikali zikiwemo; maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Maadhimisho ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa;

v. Aidha, Ofisi imeratibu shughuli za kukabiliana na maafa ikiwemo; kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa masheha wote 129 –Pemba, wanafunzi wa Skuli 14 za Dakhalia na Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Shehia;

vi. Ofisi imeimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuipatia huduma, kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo za mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na stahiki nyenginezo;

**101.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ndogo Ofisi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 764,092,544** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 583,353,080** ambazo ni sawa na **asilimia 100** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 76** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii ndogo ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 21,180,900** ikiwa ni mapato yatokanayo na vifaa vya Sherehe, hadi kufikia mwezi wa machi, 2022

Idara imekusanya jumla ya **Shilingi 2,940,000** ambayo ni sawa na **asilimia 19** kwa fedha iliyotengwa miezi tisa na **asilimia 14** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## BARAZA LA WAWAKILISHI (C02)

**103. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi lina jukumu la kutunga sheria, kufuatilia utendaji wa Serikali na kuidhinisha na kusimamia Mipango ya Maendeleo ya Serikali ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya wananchi yanapatikana. Jukumu hili la Baraza linatekelezwa kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**PROGRAMU KUU - (*CO201*): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI**

**104. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria vinatekelezwa Zanzibar ambapo matarajio ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Huduma zinazotolewa kupitia Programu hii ni pamoja na kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia taasisi za Serikali pamoja na kuidhinisha Bajeti ya Serikali.

**105. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2021 – Machi 2022) cha mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Afisi imeendelea kuratibu mikutano ya Baraza ambapo kwa kipindi hicho mikutano mitatu (3) ya Baraza ilifanyika katika miezi ya Septemba, Disemba 2021 na Februari 2022. Katika mikutano hiyo, Taarifa mbalimbali za Serikali ziliwasilishwa ndani ya Baraza, miswada kumi (10) ilijadiliwa na kupitishwa, hoja nne (4) za wajumbe zimewasilishwa na jumla ya maswali ya msingi 659 na ya nyongeza 1,458 yaliulizwa na kupata majibu ya Serikali.

ii. Afisi ya Baraza kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali iliwapatia mafunzo Wajumbe wa Baraza juu ya masuala mbali mbali, yakiwemo masuala ya uendeshaji wa shughuli za Baraza, Uchambuzi wa Miswada, Matumizi ya Tehama katika shughuli za Baraza na namna ya utafutaji rasilimali fedha.

iii. Afisi imeratibu Shughuli za Kamati ambapo Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilifuatilia utendaji wa taasisi za Serikali kwa mizunguko minne (4) katika kipindi cha (Julai- Machi) 2021/2022. Katika mizunguko hiyo, Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kamati ya Uchumi, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Kamati ya Ustawi wa Jamii, Kamati ya (PAC) na (LAAC), Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii zilifanya kazi Unguja na Pemba wakati Kamati ya maadili na kinga za wajumbe na Kamati ya Bajeti kwa pamoja zimefanya kazi Tanzania Bara.

iv. Afisi ya Baraza imeanzisha matumzi ya Baraza Mtandao kwa uendeshaji wa shughuli za Baraza pamoja na Kamati za Kudumu za Baraza ikiwa ni sehemu ya kuongeza ufanisi wa uwajibikaji katika mwaka wa fedha 2021/2022. Utumiaji wa Baraza mtandao umesaidia kupunguza gharama za matumizi ya karatasi na wino kwa Afisi ya Baraza pamoja na Serikali kupitia taarifa mbali mbali zinazowasilishwa Barazani. Aidha, mfumo huu umesaidia kuweza kuwafikishia Wajumbe taarifa kwa haraka na kwa wepesi wakiwa nje ya maeneo ya Baraza.

**PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

106. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni pamoja na kuwajengea uwezo Wajumbe na wafanyakazi, kusimamia upatikanaji wa huduma za Wajumbe na Watendaji, kuwajengea uwezo na kuimarisha mazingira ya kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

**107. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Programu hii, Afisi ya Baraza la Wawakilishi ilitekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu ambapo jumla ya wafanyakazi 13 wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya Tanzania.

ii. Afisi ya Baraza imeendelea na matengenezo mbali mbali ya jengo kwa kupaka rangi, uwekaji wa vipoza hewa (AC) kwa jengo la Afisi ya Baraza la Wawakilishi Unguja, na Kwa upande wa Afisi ya Baraza Pemba imefanya matengenezo ya ofisi na kumbi za mikutano pamoja na matengenezo ya nyumba ya Mheshimiwa Spika. Aidha, Afisi imefanikiwa kuingia kwenye Baraza Mtandao katika hatua za awali.

**108. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu zake kuu mbili kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 24,337,975,465** kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2022, Afisi imetumia jumla ya **Shilingi 12,844,441,918** sawa na **asilimia 73** kwa miezi tisa na **asilimia 53** kwa mwaka.

## TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)

**109. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**PROGRAMU KUU - (P*CO301*): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI**

**110. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2021/2022 katika Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, iliandaa uchaguzi mdogo kwa Wadi ya Chwaka uliopangwa kufanyika mwezi wa Agosti 2021. Uchaguzi huo umekuja kufuatia Tume kupokea taarifa ya kuwepo kwa nafasi ya wazi baada ya Mheshimiwa Diwani wa Wadi hiyo kufariki dunia. Hata hivyo, uchaguzi haukufanyika baada ya kujitokeza mgombea pekee kutoka Chama cha Mapinduzi, hivyo Tume ilimtangaza mgombea huyo kuwa Diwani mteule kwa mujibu wa sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2018.

ii. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Wapigakura katika shughuli mbali mbali za uchaguzi kwa asilimia 81.8. Kazi hizo hasa zimetekelezwa katika uendeshaji wa uchaguzi mdogo Wadi ya Chwaka na wakati wa zoezi la uwekaji wazi orodha za wapiga kura waliowasilisha maombi yao ya uhamisho na wapiga kura waliopoteza sifa za kuwa wapiga. Miongoni wa Shughuli hizo ni; kutoa taarifa kwa viongozi wa wilaya, kutoa taarifa kwa wananchi kwa njia ya upatu, kuendesha vipindi vya Redio na Televisheni (TV), kuendesha mikutano ya Wadau na matangazo ya kuhabarisha.

iii. Wajumbe na watendaji wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar walishiriki katika Mikutano na kazi mbalimbali ikiwa ni mwanachama wa jumuiya za kiuchaguzi za Afrika na Dunia kwa ujumla. **(Kiambatisho Nam. 7).**

iv. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa kusahihisha taarifa za Wapigakura walioomba kusahihisha taarifa zao, kuhamisha taarifa za wapiga kura kwa walioomba kuhamishiwa taarifa zao na kuwaondoa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura wale ambao wamepoteza sifa za kuwa wapiga kura ili kuliweka Daftari la Kudumu la Wapigakura katika hali ya usahihi. Pia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea kuchapisha vitambulisho vipya kwa Wapiga Kura walioharibikiwa/kupoteza vitambulisho vyao.

**PROGRAMU KUU - (*CO302*): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**111. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitekeleza kazi zifuatazo :-

i. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati 2022 – 2026 wa Afisi kufuatia kukamilika kwa muda wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa mwaka 2015-2019. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliwasiliana na Taasisi ya Kimataifa inayoshughulikia Mifumo ya Uchaguzi (The International Foundation for Electoral System - IFES) ili kuomba kupatiwa Mtaalamu mwelekezi wa kuandaa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano 2022-2026 na kuzinduliwa rasmi mwezi Febuari 2022.

ii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya shughuli mbali mbali za ufuatiliaji na Tathmini ikiwemo; Tathmini ya Mpango Mkakati wa Mwaka 2015-2019, Ufuatiliaji na Tathmini ya zoezi la Uwekaji wazi Orodha ya Wapigakura waliopoteza sifa na Wapigakura walioomba kuhamishiwa taarifa zao na Ufuatiliaji na Tathmini juu ya utekelezaji wa kazi za Afisi za Tume ya Uchaguzi Unguja na Pemba (Ofisi Kuu na Afisi za Uchaguzi za Wilaya).

iii. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imekamilisha taratibu zote zilizopelekea kuidhinishwa rasmi kwa marekebisho ya Muundo wa Taasisi (Organization Structure) wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Aidha, Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar hivi sasa tayari imeunda kamati maalum ya kuipitia rasimu ya awali ya Muundo wa Utumishi (Scheme of Service) wa Tume ya Uchaguzi kwa madhumini ya kuuweka sawa ili kuuwasilisha katika mamlaka husika kwa taratibu zaidi za Serikali.

iv. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na sekretariate yake imeweza kuendesha mikutano yake ya kawaida ya kila mwezi na ya dharura kila inapotokezea haja ya kufanya hivyo. Pia mikutano maalum ya wafanyakazi wote imekuwa ikifanyika ili kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi za ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mikutano hiyo hufanyika kila baada ya miezi mitatu.

v. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeweza kushiriki vikao mbalimbali vilivyoandaliwa na Taassisi za Serikali kujadili mambo ya uendeshaji. Vilevile, watendaji saba (7) wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika Vyuo Vikuu mbali mbali.

**112. Mheshmiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,248,900,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2022 imetumia **Shilingi 1,338,644,440** ambazo ni sawa na **asilimia 76** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 60** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka. Kwa upande wa ukusanyaji mapato ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 100,712,000** ikiwa ni faini kwa waliopoteza vitambulisho vya kupigia kura na kutengenezewa vipya ambapo hadi kufikia mwezi wa machi, 2022 Idara imekusanya jumla ya **Shilingi 402,000** ambayo ni sawa na **asilimia 0.49** kwa fedha iliyotengwa miezi tisa na **asilimia 0.4** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## UTEKELEZAJI KIFEDHA

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 51,307,882,044** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2022 imetumia **Shilingi 23,078,591,798** ambazo ni sawa na **asilimia 60** kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa na **asilimia 45 kwa** fedha zilizopangwa kutumika kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa

miradi ya maendeleo Ofisi iliidhimishiwa jumla ya **Shilingi 37,722,600,000** ambapo **Shilingi 37,622,600,000** mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hadi kufika Machi 2022 imepatiwa **Shilingi 8,556,988,256** ambazo ni sawa na **asilimia 27** kwa fedha iliyotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 23** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka **(Kiambatisho Nam. 8 na Nam. 9).**

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi vilevile ilipangiwa kukusanya **Shilingi 171,315,000** na hadi kufika Machi 2022, fedha zilizokusanywa ni **Shilingi 25,407,000** sawa na **asilimia 19** ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa miezi tisa na **aslimia 15** ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa mwaka **(Kiambatisho Namba 10).**

## MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**115.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2022/2023 itatekeleza na kusimamia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14. Kupitia Programu hizo, Ofisi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

## OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (C01)

### PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**116.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la Program hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

### Programu Ndogo - (C010101): Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais

**117.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la Program hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili

wa Rais. Matarajio ya muda mrefu ni kuimarika kwa Ofisi hii na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

118. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi kupitia Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Kuratibu ziara 60 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ndani ya nchi na ziara 2 za nje ya nchi.

ii. Kuimarisha mashirikiano na mahusiano mema ya Kitaifa na Kimataifa kwa kukutana na Mabalozi pamoja na Wageni Mashuhuri.

iii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii.

iv. Kuyafanyia kazi malalamiko, migogoro na kero za wananchi kwa kushirikiana na taasisi husika.

v. Kufanya matengenezo katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais yaliyoko Dodoma, Pemba na Unguja.

vi. Kuratibu na kufanya vikao vya uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Wizara zote za SMZ ambacho kitafanyika kila baada ya miezi mitatu.

vii. Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi watano (5) wa Ofisi ya Faragha kwa kiwango cha Stashahada na Cheti pamoja na kuwapatia stahiki za likizo wafanyakazi.

119. **Mheshimiwa Spika,** mgao wa fedha kwa Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2022/2023 imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 1,708,067,126** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 825,383,836** ni kwa ajili ya malipo ya mshahara na **Shilingi 882,683,290** ni kwa matumizi mengineyo.

## PROGRAMU KUU - (C0102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

**120. Mheshimiwa Spika,** programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu wa uratibu wa shughuli za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kupatikana kwa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina programu ndogo nne (4).

### Programu Ndogo – CO10201: Kukabiliana na Maafa

**121. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya kutokea. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar.

**122. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamisheni imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu utoaji wa huduma na misaada ya kibinaadamu kwa matukio mbalimbali ya majanga yatakayotokea Unguja na Pemba;

ii. Kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa makundi mbalimbali ya jamii pamoja na taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali;

iii. Kufanya zoezi la utayari wa kijiandaa na kukabiliana na matukio ya majanga na maafa yanayoweza kutokea;

iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli zote zinazotekelezwa na Kamisheni katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia;

v. Kuandaa mikutano na wahusika mbalimbali wa masuala ya kukabiliana na maafa katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia;

vi. Kuimarisha Mfumo wa Mawasiliano ya Dharura kwa kufanya matengenezo ya mitambo ya mawasiliano na kuwajengea uwezo watendaji wanaosimamia mfumo huo-;

vii. Kutoa taarifa za tahadhari za mapema kwa jamii juu ya majanga mbalimbali yanayoweza kutokea;

viii. Kufanya ukaguzi katika maeneo 18 yanayotoa huduma kwa jamii kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa mipango na taratibu za kukabiliana na maafa katika maeneo hayo;

ix. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wanne (4) Unguja na Pemba;

**123.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu mbili (2); (a) Programu ya Kuijengea Uwezo Jamii katika Kujikinga na Kukabiliana na Maafa na (b) Programu ya Kutokomeza Kipindupundu Zanzibar na imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya kukabiliana na maafa pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na maafa katika ngazi za Shehia, Wilaya na Taifa kwa Unguja na Pemba;

ii. Kuimarisha mfumo wa mawasiliano utakaorahisisha utoaji na upokeaji wa taarifa za maafa katika ngazi zote;

iii. Kuimarisha ghala za vifaa vya kukabiliana na maafa kwa kununua vifaa vya huduma za kibinaadamu na kukabiliana na maafa;

iv. Kuimarisha mfumo wa kielektoniki wa kutunza takwimu za matukio ya majanga na maafa yanayotokea;

v. Kuhamasisha jamii kutoa taarifa sahihi na kwa wakati pindi yanapotokea maafa;

vi. Kuandaa miongozo mbalimbali ya kukabiliana na maafa katika ngazi za Shehia, Wilaya na Taifa;

vii. Kuimarisha vituo vya operesheni na mawasiliano ya dharura vilivyopo Maruhubi, Gamba na Makunduchi kwa Unguja na Mkoani, Chake Chake na Micheweni kwa Pemba;

viii. Kuimarisha Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari za Mapema na kinga dhidi ya maafa;

ix. Kuainisha na kuandaa ramani ya maeneo hatarishi (Disaster zones).

**124. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 1,693,842,758** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 479,700,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,214,142,758 (755,000,000** kutoka SMZ na **459,142,758** kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – CO10202: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa**

**125. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi kupitia Programu ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu Sherehe za miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

ii. Kuratibu ushiriki wa Wananchi na Viongozi katika Maadhimisho ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara.

iii. Kulifanyia matengenezo makubwa kaburi la aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar na Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume.

iv. Kuratibu Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi na Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume.

v. Kununua bendera kwa ajili kuuza na bendera za jeneza kwa ajili ya maziko ya Viongozi wa Kitaifa.

vi. Kukamilisha matengenezo ya uzio wa jengo la Ofisi ya Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa liliopo Mwanakwerekwe.

vii. Kununua vifaa vya sherehe ikiwemo, mashamiana, viti, meza na bendera kwa ajili ya Sherehe za Kitaifa.

viii. Kuimarisha huduma za usafiri kwa kununua gari kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

ix. Kuendelea kumpatia mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja (1) wa Idara pamoja na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili (2) wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho Kitaifa.

x. Kuimarisha utendaji wa Ofisi kwa kununua vifaa mbali mbali vya kufanyia kazi vikiwemo karatasi, mafuta na vifaa vya kuandikia.

**126. Mheshimiwa Spika,** Ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2022/2023, tunaomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 1,280,991,281** ambapo **Shilingi 216,700,920** kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na **Shilingi 1,064,290,361**kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – CO10203: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**127. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, mambo ya muungano, utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala 2020 – 2025; uratibu wa baraza la Wawakilishi, uratibu wa masuala ya utafiti na uratibu wa utekelezaji wa Mfuko wa maendeleo ya Jimbo;

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya sera,

iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya muungano ikiwemo uratibu na uandaaji wa vikao vya masuala ya muungano, uratibu wa masuala ya muungano Zanzibar na ushirikiano baina ya SMZ na SMT;

iv. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Zanzibar (TASAF),

v. Uendeshaji wa shughuli na matumizi ya Idara.

**128. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III), Ofisi itaendelea kutekeleza Shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kusimamia uibuaji wa Kaya Maskini;

ii. Kuratibu na kusimamia uhaulishaji wa fedha za ruzuku kwa kaya masikini katika Shehia za Unguja na Pemba;

iii. Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira ya muda kwa Walengwa wa Mpango;

iv. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu ikiwemo ya Afya, Maji na Elimu;

v. Kutoa mafunzo mbalimbali kwa Walengwa, Watendaji na viongozi wanaosimamia Shughuli za TASAF;

vi. Kuandaa vikao viwili vya Kamati ya Uongozi (Steering Committee);

vii. Kuandaa vikao viwili vya Kamati Tendaji (Management Committee);

viii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa TASAF baina ya Zanzibar na Tanzania bara;

ix. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya TASAF Zanzibar;

x. Kusimamia uendeshaji wa Ofisi kwa Shughuli za TASAF Unguja na Pemba;

xi. Kuratibu na kusimamia vikundi vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya; na

xii. Kuratibu na kusimamia Mipango ya Biashara kwa Walengwa wa TASAF.

**129. Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 31,596,156,918** ambapo **Shilingi 434,505,528** kwa ajili ya Mshahara, **Shilingi 298,017,140** matumizi ya kawaida, **Shilingi 100,000,000** zikiwa ni mchango wa SMZ katika Programu ya TASAF na **Shilingi 14,644,434,250** ni mchango wa washirika wa Maendeleo katika Programu ya TASAF. Aidha, **Shilingi 16,119,200,000** ni ruzuku kwa ajili Idara ya Uhamiaji Zanzibar.

**Programu Ndogo – CO10204: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Dodoma**

**130. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dodoma ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Taasisi/Wizara za SMZ na SMT, Washirika wa Maendeleo, Afisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa ikiwemo kuimarisha na kuibua maeneo mapya ya uhusiano na ushirikiano.

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu na kushiriki vikao 80 vya Ofisi na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

ii. Kuratibu na kushiriki vikao vya kisekta baina ya Wizara na Taasisi za SMZ na Wizara na Taasisi za SMT.

iii. Kutoa elimu juu ya uwepo wa ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma kwa kuandaa vipindi viwili (2) vya Television, kuandaa warsha kwa wadau mbali mbali, kufanya utafiti juu utoaji wa huduma za ofisi ya Uratibu Dodoma, kushiriki katika tamasha la biashara la saba saba, tamasha la biashara ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na kuandaa kongamano la Sherehe ya Mapinduzi ya Zanzibar.

iv. Kutoa huduma kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapokuwa Tanzania Bara kwa kuwapatia huduma za Usafiri na uratibu wa huduma za upatikanaji wa Viza.

v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo kwa kwenda kujifunza katika Wizara na Taasisi za Tanzania Bara.

vi. Kulipia huduma na vifaa vya Ofisi.

vii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili (2) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wawili (2) na kuwapatia wafanyakazi wote stahiki nyengine.

132. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dodoma itekeleze malengo yake hayo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,158,562,041** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 417,850,560** kwa malipo ya mishahara ya **Shilingi 740,711,481** kwa matumizi mengineyo.

**PROGRAMU KUU - (PCO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

133. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Afisi ili kutoa huduma bora kwa jamii. Programu hii kuu ina Programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Afisi, Pemba.

**Programu Ndogo – CO10401: Uongozi na Utawala**

134. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia na kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora za uendeshaji za kila siku pamoja na kusimamia maslahi na rasilimali za Ofisi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu ndogo ya Uongozi na Utawala pamoja na mambo mengine, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo mishahara na stahiki nyinginezo kwa mujibu wa taratibu;

ii. Kuratibu na kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika kada na ngazi mbalimbali ndani na nje ya Tanzania kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi;

iii. Kuratibu na kusimamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi;

iv. Kuratibu na kusimamia vikao vya utendaji kazi vya Ofisi vikiwemo vya Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji;

v. Kutoa huduma za ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil; kwa ajili ya mikutano mbalimbali kwa Taasisi za Serikali na Binafsi.

vi. Kutoa mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2014 pamoja na matoleo mbali mbali ya kiutumishi kwa watumishi wa Ofisi;

vii. Kutoa mafunzo ya kujiandaa kustaafu kazi (pre-retirement training) kwa watumishi wanaotarajiwa kustaafu kazi,

viii. Kuandaa Mpango wa Uandaaji Uongozi (Succession Plan) wenye kuzingatia sifa na taaluma za watumishi (Mentor and coaching),

ix. Kuimarisha miundombinu salama ya uokozi katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**135. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,629,249,800** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 663,534,672** ni kwa malipo ya mshahara na **Shilingi 965,715,128** kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – CO10402: Mipango, Sera na Utafiti**

**136. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na kuandaa na kusimamia mipango na bajeti na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti, mipango ya Ofisi pamoja na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

ii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Stretegic Plan) 2022-2027;

iii. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu/ miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara/Taasisi zilizozo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

iv. Kuratibu uandaaji wa mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo inayohusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

v. Kuratibu na kuandaa Vikao vya Mashirikiano baaina na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mambo ya Ndani za SMT;

vi. Kufanya mafunzo juu ya uandaaji wa bajeti kwa maafisa mipango wa Idara/Taasisi zilizopo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

vii. Kujenga uwezo kwa Maafisa Ufuatiliaji na tathmini Mipango wa Idara/Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya ufuatiliaji na tathimini wenye kutoa matokeo (Results Base Monitoring and Evaluation);

viii. Kuwajengea uwezo wa uandaaji wa Sera kwa Maafisa Sera wa Idara/Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

ix. Kuandaa maandiko ya muhtasari wa tafiti (Policy Briefs) na kujadili matokeo ya tafiti zilizofanywa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na kutafuta fursa za fedha kwa ajili ya miradi ya tafiti.

x. Kuanzisha Mfumo wa kuhifadhia taarifa za Takwimu (Statistical Database) na kuandaa nyenzo za kukusanya taarifa za takwimu za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

xi. Kuratibu na kuandaa Mpango Mkakati wa Takwimu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

xii. Kusimamia shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM).

xiii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu (3) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi watano (5) mafunzo ya muda mfupi.

**137. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga Kutumia jumla ya **Shilingi 485,749,101** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 186,898,860** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 298,850,241** ni kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – CO10403: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba**

**138. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba inahusika na kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba kwa kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi. Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

ii. Kuratibu ziara na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais;

iii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi saba (7) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi watatu (3);

iv. Kuandaa mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

v. Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji

wa Program ya Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali Pemba;
vii. Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa;

viii. Kuratibu maadhimisho ya sherehe za kutimia miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Maadhimisho ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

139. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba itekeleze hayo kwa mwaka 2022/2023, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 925,075,225** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 634,485,624** kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho maalum na mchango wa ZSSF na **Shilingi 290,589,601** kwa matumizi mengineyo.

## BARAZA LA WAWAKILISHI (C02)

140. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi linatekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu Kuu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

141. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada

ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali.

**142. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Baraza na Afisi.

**143. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hizi limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuratibu mikutano minne (4) ya kila mwaka ya Baraza la Wawakilishi.

ii. Kuratibu shughuli za Kamati za kudumu za Baraza.

iii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kukuza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

iv. Kuendelea kutoa taaluma kwa umma kuhusu shughuli za Baraza kupitia vipindi vya Redio na Televisheni .

v. Kuendelea kuimarisha mazingira ya Baraza kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya Majengo.

vi. Kuanza matayarisho ya utanuzi wa Jengo la Afisi ya Baraza ili kuondoa changamoto ya uhaba wa nafasi.

**144. Mheshimiwa Spika,** ili Afisi ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza malengo yake hayo kwa ufanisi zaidi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 24,674,700,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 8,940,194,460** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 15,734,505,540** ni kwa kazi nyenginezo.

## TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)

**145. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inasimamia Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**PROGRAMU KUU - (CO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI**

**146. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2022/2023 Tume ya Uchaguzi itaendelea kutekeleza Programu zake za msingi za Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Usimamizi wa Kazi za utawala na Uendeshaji wa shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**147.** Katika Programu ya uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi imekusudia kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendeleza Daftari la Kudumu wa Wapiga Kura.

ii. Kuendelea kutoa elimu ya wapiga kura kwa makundi mbali mbali.

iii. Kuendesha Uchaguzi Mdogo utakapojitokeza.

iv. Kufanya mapitio ya sheria na kanuni zinazohusiana na Afisi na uendeshaji wa uchaguzi.

**148. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi fedha zake zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**PROGRAMU KUU - (CO301): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**149. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2022/2023 Tume ya Uchaguzi itaendelea kutekeleza

Programu zake za msingi za Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Usimamizi wa Kazi za utawala za Uendeshaji wa shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Kupitia Programu hii Afisi ya Tume ya Uchaguzi, imekusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kununua vifaa pamoja na huduma mbali mbali kwa ajili ya kuleta ufanisi katika Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

ii. Kuendelea kutoa fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa wafanyakazi katika ngazi mbali mbali za elimu.

iii. Kuimarisha majengo ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

iv. Kutoa elimu ya Uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

v. Kujenga majengo mapya ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**150.** **Mheshimiwa Spika,** ili Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iweze kutekeleza malengo ya Program zake naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,216,530,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,412,600,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 803,930,000** ni kwa kazi nyenginezo.

**UKUSANYAJI MAPATO**

**151.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 92,826,495** kwa mchanganuo ufuataao:-

| | |
|---|---|
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 52,710,000 |
| Afisi Kuu Pemba | 22,542,495 |
| Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 17,574,000 |
| **Jumla** | **92,826,495** |

**152. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Programu zote 7 za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni jumla ya **Shilingi 67,368,924,250. Shilingi 14,211,854,460** kwa ajili ya mshahara, **Shilingi 38,412,635,540** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 14,744,434,250** kwa miradi ya maendeleo **(Kiambatisho Nam. 11).** Na kwa upande wa makusanyo ni **Shilingi 92,826,495.**

**HITIMISHO**

**153. Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu hii ya bajeti, naomba sasa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini ambayo imekuwa karibu sana na Ofisi yetu katika kutuelekeza na kutushauri juu ya utekelezaji wa majukumu yetu. Naishukuru sana kwa kuipokea, kuipitia na hatimae kuridhia hotuba hii kuwasilishwa katika Baraza hili. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itaendelea kufanyakazi na Kamati hii kwa ukaribu zaidi katika kuwatumikia wananchi.

**154. Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza miango yake ikiwemo washirika wa maendeleo. Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wenzetu hawa kwa kuendelea kutuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo. Miongoni mwa washirika hao ni:- Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, UNAIDS, USAID, FAO, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI, Nchi za China, India, Japan, Marekani, Oman, Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE), BADEA, GPE, KOICA, Sida- Sweden Shirika la Good-neighbours la Korea, AfDB, Cuba, Milele Zanzibar Foundation, Asasi za kiraia na wengine wote

wanaoshirikiana nasi. Tunaahidi kuendelea kushirikiana nao kwa mwaka ujao wa fedha na miaka mingine na tunawaomba waendelee kutuunga mkono katika utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja harakati zetu za kuimarisha uchumi na kuleta maendeleo ya watu wetu na nchi kwa jumla.

155. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kitaifa tumekuwa tukishirikiana kwa karibu sana na taasisi na mashirika yasio ya kiserikali pamoja na wafanyabiashara kwa kuwahudumia wananchi katika nyanja mbalimbali. Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wadau wetu hao kwa moyo wao wa uzalendo na nawaomba waendelee na moyo wao huo kadri hali itakavyoruhusu. Na sisi Serikali kwa upande wetu tutaendelea kuweka mazingira mazuri ili waendelee kufanya kazi zao kwa usalama na amani.

156. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi yetu imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nichukue nafasi hii kuzishukuru kwa dhati Ofisi hizi kwa namna tunafanya kazi kwa pamoja katika kuratibu masuala mbalimbali ya kitaifa.

157. **Mheshimiwa Spika,** sitoacha kuwashukuru sana wenzetu wa vyombo vya habari vya Serikali na binafsi kwa namna wanvyoshikiana na Serikali katika kuwahabarisha, kuwaelimisha na kuwaburudisha wananchi. Hakika wameendelea kuifanya kazi yao kwa weledi mkubwa katika kujenga nchi yetu. Nawaomba waendelee kushirikiana na Serikali ili kutoa taarifa za uhakika.

158. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi yetu napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Hamza Hassan Juma kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na pili namshukuru kwa mashirikiano makubwa anayonipa katika usaidizi wa kuiongoza Ofisi

yetu. Namuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu na uwezo wa kutekeleza vyema majukumu yake mapya aliyokabidhiwa. Lakini pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa kuisimamia vyema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi chote alichokuwa nasi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naamini ataendeleza vyema weledi na uwezo wake aliounesha katika Ofisi yetu katika kutumikia nafasi yake mpya aliyokabidhiwa. In sha Allah, Mwenyezi Mungu atamsaidia katika kutekeleza vyema majukumu yake mapya.

159. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Thabit Idarous Faina pamoja na timu yake ya Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi/Idara kwa kusimamia vyema mipango na utekelezaji wa kazi za Ofisi yetu. Uwajibikaji wao umewezesha Ofisi hii kufikia malengo yake kwa ufanisi mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwangozea nguvu na maarifa zaidi ya kutekeleza kazi zao kwa manufaa ya nchi yetu.

160. **Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu, bajeti hii ya Ofsi yetu nimeisoma tukiwa katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan, hivyo sina budi kuwakumbusha waislamu wenzangu wote kuwa tukithirishe kufanya ibada pamoja na kwa wale wenye uwezo kuwasaidia wasiojiweza. Vile vile, napenda kuwakumbusha kujiepusha na mambo yote yanayobatilisha swaumu ili tuweze kufikia lengo la funga zetu. Kwa upande wa wafanyabiashara napenda niwakumbushe kuwa Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa neema hivyo waitumie neema hiyo kwa kuuza bidhaa zao kwa bei nafuu kama zilivyoelekezwa na mamlaka za Serikali kwa faida yetu sote. Aidha, napenda kuwasisitiza wafanyabiashara wetu wote kulipa kodi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa bila ya kusahau kutoa risiti kwa wanaowahudumia. Kwa upande wa Wananchi wenzangu nawakumbusha kuendelea kudai risiti kila wanapopatiwa huduma kutoka kwa wafanyabiashara ili kuimarisha mapato ya nchi yetu.

161. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 67,368,924,250** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 nilizozielezea hapo awali. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| C01 - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | **Shilingi** | **40,477,694,250** |
| C02 - Afisi ya Baraza la Wawakilishi | **Shilingi** | **24,674,700,000** |
| C03 - Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | **Shilingi** | **2,216,530,000** |
| **JUMLA KUU** | **Shilingi** | **67,368,924,250** |

162. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHE. HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**

**Kiambatisho Nam. 1**

**Ziara Za Mheshimiwa Makamu Wa Pili Wa Rais Wa Zanzibar Oktoba – Disemba 2021/2022**

| Nam | Shughuli | Tarehe | Pahali |
|---|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais atembelea maeneo ya Shangani – African House na Tumekuja | 22/10/2021 | Shangani – African House na Tumekuja |
| 2. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alitembelea maeneo ya Mpiga Duri | 25/10/2021 | Maeneo ya Mpiga Duri |
| 3. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mbiundombinu ya maji | 17/11/2021 | Dole, Masingini, Kwarara na Maungani |
| 4. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara ya kuzikagua hoteli nne zilizoathiriwa na janga la moto | 21/11/2021 | Jambiani KIbigiji, Mkoa wa Kusini Unguja |
| 5. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya Ujenzi wa Miradi ya kilimo cha umwagiliaji katika bonde ya Cheju na Kibokwa | 22/11/2021 | Cheju na Kibokwa |
| 6. | Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara ya kutembelea katika kiwanda cha kutengeneza kanga na Matenge Basra Textile Limited | 29/11/2021 | Chumbuni |
| 7. | Ziara ya ukaguzi wa bomba la maji lililopasuliwa na mkandarasi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya katika eneo la Skuli ya Lumumba | 25 Januari 2022 | Lumumba Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi. |
| 8. | Ziara ya ukaguzi wa shughuli za uingizaji na usambazaji wa dawa katika Bohari kuu ya madawa. | 25 Januari 2022 | Maruhubi – Wilaya Mjini Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi. |
| 9. | Ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa tangi la maji katika sehia ya kidanzini | 25 Januari 2022 | Bumbwini Wilaya ya Kaskazini B |
| 10. | Ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini B | 25 Januari 2022 | Pangatupu – Wilaya ya Kaskazini B Mkoa wa Mjini Magharibi |
| 11. | Ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini A Unguja. | 25 Januari 2022 | Kivunge – Wilaya ya Kaskazini A ' Mkoa wa Kaskazini Unguja |
| 12. | Ziara ya kukagua mradi wa ukarabati waw a Skuli ya Uzini | 25 Januari 2022 | Uzini Wilaya ya Kati Mkoa Kusini Unguja |
| 13. | Ziara ya kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa skuli Mjumuisho | 25 Januari 2022 | Jendele Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja |

| Nam | Shughuli | Tarehe | Pahali |
|---|---|---|---|
| 14. | Ziara ya kutembelea na kukagua ujenzi wa mradi wa Skuli ya Maandalizi Unguja Ukuu | 25 Januari 2022 | Unguja Ukuu Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja |
| 15. | Ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa Skuli ya mwanakwerekwe D na G | 26 Januari 2022 | Mwanakwerekwe |
| 16. | Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Magharibi B | 26 Januari 2022 | Mwanakwerekwe ijitimai – Wilaya ya Magharibi B |
| 17. | Ziara ua ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mjini Magharibi. | 26 Januari 2022 | Lumumba – Wilaya ya Mjini |
| 18. | Ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mjini | 26 Januari 2022 | Chumbuni Wilaya ya Mjini |
| 19. | Zuiara ya ukaguzi eneo la Ujenzi wa skuli | 26 Januari 2022 | Magufuli – Wilaya ya Magharibi A |
| 20. | Ziara ya Ukaguzi wa eneo la ujenzi wa madarasa katika skuli ya Masingini | 26 Januari 2022 | Masingini – Wilaya ya Magharibi A |
| 21. | Ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Magharibi A | 26 Januari 2022 | Mbuzini – Wilaya ya Magharibi A |
| 22. | Ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa madarasa saba 7 ya mfano Skuli ya Ng'ombeni | 12 Februari 2022 | Ngombeni - Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba |
| 23. | Ziara ya kukagua Zoezi la Ufungaji wa Mashine ya CT Scan katika hospitali ya Abdalla Mzee | 12 Februari 2022 | Mkoani -Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba |
| 24. | Ziara ya kukagua Mradi wa ujenzi wa skuli ya Mwambe | 12 Februari 2022 | Mwambe Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba |
| 25. | Ziara ya ukaguzi wa Mradi wa ujenzi wa kuli ya Pujini | 12 Februari 2022 | Pujini – Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba |
| 26. | Ziara ya kukagua Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake | 12 Februari 2022 | Vitongoji– Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba |
| 27. | Ziara ya kukagua Bohari Kuu ya Madawa | 12 Februari 2022 | Vitongoji – Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba |
| 28. | Ziara ya kukagua Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Kwale | 12 Februari 2022 | Kwale – Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba |
| 29. | Ziara ya kukagua Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Micheweni | 13 Februari 2022 | Micheweni – Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba |
| 30. | Ziara ya kukagua Mradi wa Skuli ya Makangale | 13 Februari 2022 | Makangale – Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba |
| 31. | Ziara ya ukaguzi wa Mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Wete | 13 Februari 2022 | Kinyasini – Wilaya ya Wete Mkoa wa |

| Nam | Shughuli | Tarehe | Pahali |
|---|---|---|---|
| | | | Kaskazini Pemba |
| 32. | Ziara ya ukaguzi Mradi wa ujenzi wa Skuli ya Maziwani | 13 Februari 2022 | Maziwani– Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba |
| 33. | Ziara ya eneo lilipokumbwa na kuathiriwa na upepo wa kimbunga uliotokea siku ya Jumanne tarehe 22/03/2022 | 23 Marchi 2022 | Kendwa – Wilaya ya Kaskazini A Mkoa wa Kaskazini Unguja |

Kiambatisho Nam. 2

**Hoja Zilizoondolewa kwenye Orodha ya Hoja za Muungano na Kusainiwa Hati za Makubaliano**

| NAM. | HOJA | CHIMBUKO LA HOJA | UFUMBUZI |
|---|---|---|---|
| 1. | Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu | Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ilikuwa haitekelezwi Zanzibar kutokana na kutozihusisha taasisi za SMZ zinazoshughulikia masuala ya Uvuvi katika Bahari Kuu. | Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwezi Februari, 2007 kupitia Sheria Na. 4 ya mwaka 2007 na kuzitambua taasisi zinazohusika na matumizi ya Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar na kuzijumuisha katika Kamati ya Utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Sambamba na marekebisho ya Sheria, hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kufunguliwa kwa akaunti ya amana kwa ajili ya kuweka mapato yatokanayo na shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu, kufikiwa kwa makubaliano ya kugawana mapato kuwa, asilimia 50 ni kwa jajili ya uendeshaji wa Mamlaka ya Uvuvi na asilimia 50 itaganywa kwa asilimia 30 Tanzania Bara na asilimia 20 Zanzibar. Mkubaliano mengine ni mgao wa wafanyakazi wa Mamlaka kwa pande zote za Muungano.<br><br>Kadhalika, Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020 ilitungwa na Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria hiyo imeorodheshwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 23 Februari, 2021. |
| 2. | Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar | Kikwazo cha kuzuiwa kwa maziwa ya AZAM kuingia katika soko la Tanzania Bara | Maziwa ya AZAM yameanza kuingia katika soko la Tanzania Bara baada ya Kanuni kufanyiwa marekebisho, ikiwa ni pamoja na kupunguziwa tozo kutoka shilingi 2000 hadi |

| NAM. | HOJA | CHIMBUKO LA HOJA | UFUMBUZI |
|---|---|---|---|
| | | kinachotokana na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura ya 156 na Kanuni zake kwa upande wa Tanzania Bara. | shilingi 250 kwa lita ya maziwa yanayotengenezwa kutokana na unga wa maziwa unaoagizwa nje ya nchi. Vilevile, Tarehe 25 Februari, 2019 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) - SMT iliingia Mkataba wa Makubaliano ya uingizaji wa maziwa ya AZAM katika soko la Tanzania Bara. |
| 3. | Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano | Kupungua kwa kiwango cha ushindani katika soko la ajira kwa Wazanzibari kunatokana na tofauti ya mitaala ya elimu ya msingi na sekondari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Suala jengine ni kuendeleza Ari na Dhamira ya Muungano katika kufanya uteuzi wa nafasi mbalimbali katika Taasisi za Muungano. | Kamati ya Kukuza Mitaala iliyoundwa ikiwa na wajumbe kutoka pande mbili za Muungano ililinganisha mihutasari ya ngazi zote za elimu (Msingi hadi Vyuo) ya Tanzania Bara na Zanzibar na kubaini kuwa tatizo sio tofauti ya mitaala bali ni nafasi ya Wazanzibari katika Taasisi za Muungano.<br>Hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kutatua changamoto zikiwemo kuhamasisha Wazanzibari kuomba ajira zinazotangazwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Taasisi za Muungano; Matangazo ya ajira kutangazwa kupitia vyombo vya habari vya Tanzania Bara na Zanzibar; Taasisi za Muungano kufungua Ofisi Zanzibar ikiwa ni pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na usaili kufanyika Zanzibar pia.<br>Utaratibu wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika kuhusu nafasi za Watumishi wa kawaida kwenye Taasisi za Muungano (isipokuwa kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama) ni asilimia 79 kwa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Tanzania Zanzibar. Pia, SMT na SMZ zimekubaliana kuwa na mfumo shirikishi katika mchakato mzima wa ajira katika Taasisi za Muungano na sasa wafanyakazi wa SMZ wamepelekwa Sekretarieti ya Ajira. |
| 4. | Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kibajeti (General Budget Support – GBS) | Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kibajeti ni asilimia 95.5 kwa SMT na asilimia 4.5 kwa SMZ ambapo | Utaratibu wa kupokea fedha za misaada ya kibajeti ya kisekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeelekezwa kwenye kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na |

| NAM. | HOJA | CHIMBUKO LA HOJA | UFUMBUZI |
|---|---|---|---|
| | | mgawanyo huu ndiyo unaotekelezwa hadi sasa. Hata hivyo, suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kibajeti ya kisekta bado halijafanyiwa kazi. | Misaada Sura 134, ambapo SMZ ina jukumu la kupokea misaada hiyo bila kutafuta idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango wa SMT. |
| 5. | Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na mkataba huo kuwa na kipengele Na. 4.01 ambacho kinaitaka Serikali iweke baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo. | Baada ya mazungumzo baina ya SMT na mkopeshaji kuhusu kipengele Na. 4.01, mtoa mkopo alikubali mapendekezo ya kufanya marekebisho katika kipengele hicho kilichohusu kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo. Hivyo, Serikali ilisaini mkataba huo tarehe 19 Aprili, 2020 baada ya kuondolewa kwa kipengele hicho. |
| 6. | Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba | Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba kutokana na mkataba huo kuwa na kipengele Na. 4.01 ambacho kinaitaka Serikali iweke baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo. | Baada ya mazungumzo baina ya SMT na mkopeshaji kuhusu kipengele Na. 4.01, mtoa mkopo alikubali mapendekezo ya kufanya marekebisho katika kipengele hicho kilichohusu kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo huo kwa kuondoa kipengele hicho. Hivyo, Serikali ilisaini mkataba huo tarehe 19 Aprili, 2020. |
| 7. | Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri | Kuchelewa kukamilishwa kwa Mkataba wa Mkopo kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. | Serikali iliunda Timu ya wataalamu ili kupitia upya Andiko la Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Pamoja na mambo mengine, Timu hiyo ilibaini kuwa andiko la mradi liliandaliwa na kampuni ambayo ni mkandarasi tarajiwa wa mradi kwa mujibu wa hati ya makubaliano (MoU) ya mwaka 2012 baina ya kampuni hiyo na SMZ. Suala hili lingeweza kusababisha mgongano wa kimaslahi. Hivyo Timu ilishauri andiko la mradi liandaliwe na mtaalamu elekezi huru ili kuepusha mgongano wa kimaslahi. |

| NAM. | HOJA | CHIMBUKO LA HOJA | UFUMBUZI |
|---|---|---|---|
| | | | Baada ya ushauri huo, SMZ ilisitisha makubaliano na kampuni hiyo na kutafuta mtaalamu elekezi huru wa kuandaa andiko jipya. |
| 8. | Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (Zanzibar Revenue Board - ZRB) | Baada ya kuzimwa mfumo uliokuwa unatumika kukokotoa kodi kwenye huduma za simu (Electronic Revenue Collection System - e-RCS) ambao ulikuwa unatumika kukusanya na kugawana kodi baina ya pande mbili za Muungano, ZRB iliendelea kutumia mfumo huo kukusanya kodi jambo lililoleta malalamiko kutoka kwa Kampuni za Simu. | Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT na SMZ zimefanya maboresho ya Mfumo wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye huduma za simu. Hivyo, mfumo ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Januari, 2020. |
| 9. | Mapato Yanayokusanywa na Uhamiaji kwa Upande wa Zanzibar | Mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar yanapaswa kuwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti na kutumika katika kugharamia shughuli za Muungano kulingana na bajeti zilizotengwa. Hivyo, mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji upande wa Zanzibar ambayo yanabakizwa Zanzibar ni kinyume na Sheria ya bajeti. | Katika hotuba ya bajeti 2021/22 iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Mipango (SMT) tarehe 10 Juni, 2021 ilipendekezwa kutekeleza utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na Tozo za VISA kutumika pale yalipokusanywa kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano. Mapendekezo haya yalipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Juni 2021. |
| | **Hoja za Kiutendaji Zilizoondolewa Kwenye Orodha ya Hoja za Muungano Ambazo Hazikusainiwa Hati za Makubaliano** | | |

| NAM. | HOJA | CHIMBUKO LA HOJA | UFUMBUZI |
|---|---|---|---|
| 10. | Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Tanzania Revenue Appeal Tribunal (TRAT) kutoka Zanzibar | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchelewa kuwasilisha jina kwa ajili ya uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa TRAT. | Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa TRAT ulifanyika tarehe 24 Aprili, 2019. |
| 11. | Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board - DIB) kutoka Zanzibar | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchelewa kuwasilisha jina kwa ajili ya uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana. | Uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana ulifanyika tarehe 22 Machi, 2019. |

**Kiambatisho Nam. 3**

**Wizara Zilizofanya Vikao vya Ushirikiano kwa Mwaka wa Fedha 2021/22**

| NA. | WIZARA | TAREHE YA KIKAO |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (SJMT) na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) | 1 Julai, 2021 |
| 2. | Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT) na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) | 2 Julai, 2021 |
| 3. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (SJMT) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (SMZ) | 9 Julai, 2021 |
| 4. | Wizara ya Madini (SJMT) na Wizara ya Maji, Nishati na Madini (SMZ) | 26 Julai, 2021 |
| 5. | Wizara ya Nishati (SJMT) na Wizara ya Maji, Nishati na Madini (SMZ) | 9 – 10 Agosti, 2021 |
| 6. | Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (SJMT) na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ) | 2 - 5 Agosti, 2021 |
| 7. | Wizara ya Fedha na Mipango (SJMT) na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango (SMZ) | 4 Agosti, 2021 |

| NA. | WIZARA | TAREHE YA KIKAO |
|---|---|---|
| 8. | Wizara ya Madini (SJMT) na Wizara ya Maji, Nishati na Madini (SMZ) | - 12 11 Agosti, 2021 |
| 9. | Wizara ya Katiba na Sheria (SJMT) na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) | 11 Agosti, 2021 |
| 10. | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SJMT) na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) | 8 – 10 Septemba, 2021 |
| 11. | Wizara ya Maliasili na Utalii (SJMT) na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (SMZ) | 27 – 30 Septemba, 2021 |
| 12. | Wizara ya Nishati (SJMT) na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (SMZ) | 27 Oktoba, 2021 |
| 13. | Wizara ya Maji (SJMT) na Wizara ya Maji, Nishati na Madini (SMZ) | 25 – 27 Novemba, 2021 |
| 14. | Wizara ya Mifugo (SJMT) na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (SMZ) | 29 Novemba, 2021 |
| 15. | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) ya SJMT na (SMZ) | 10 Disemba, 2021 |
| 16. | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SJMT) na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) | 12 - 15 Disemba, 2021 |
| 17. | Wizara ya Utamaduni na Michezo (SJMT) na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (SMZ) | 13 – 14 Januari, 2022 |

**Kiambatisho Nam. 4**

**Taarifa za Mikutano/Vikao Vilivyohudhuriwa kwa Kipindi cha Jalai hadi Machi**

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | 21 – 25/07/2021 | Mkutano wa 17 wa Baraza la kisekta katika Usafirishaji, Mawasiliano na Hali ya Hewa.<br>(The 17th Meeting of the Sectorial Council on Transport, Communication and Meteorology). | Mkutano huu umefanyika katika Hoteli ya Four Point jijini Dar es Salaam ambao ulilenga katika kupitia utekelezaji wa maamuzi ya sera ya taasisi na kupitia hatua za kimaendeleo za miradi zilizochukuliwa na taasisi husika katika jumuia ya Afrika Mashariki.<br>Mkutano huo ulifanyika katika ngazi tatu ikiwemo ngazi ya Wataalam (Technical personnel), Ngazi ya Makatibu Wakuu na kumalizia ngazi ya Mawaziri ambao waliidhinisha na kuweka sahii ripoti iliyoandaliwa katika Mkutano huo. |
| 2. | 01/07/2021 | Kikao cha maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Tume ya pamoja ya kudumu ya ushirikiano (JPC) kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika chuo kikuu cha Dodoma (informatics). Kikao hicho kililenga katika kufanya maandalizi ya kikao cha Pili cha mashirikiano ambacho kilipendekezwa kufanyika Tanzania. Kikao kiliwataka wajumbe kuainisha maeneo muhimu ambayo Tanzania kupitia secta zake itapendelea kushirikiana na nchi zilizomo katika Umoja wa Falme za Kiarabu. |
| 3. | 01/07/2021 | Kikao cha mashirikiano ngazi ya Makatibu wakuu kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu SMT na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais SMZ. | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Lengo kuu la kikao hicho ilikua ni kutimiza matakwa ya viongozi wa kuu wan chi pamoja na miongozo yake ya kuzitaka taasisi za SMT na SMZ kukutana mara kwa mara ili kujadili utekelezaji wa |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | | mambo mbali mbali kwa maslahi ya nchi. Aidha kikao pia kililenga kutimiza matakwa ya katiba za nchi husika sambamba na kukidhi tunu za Muungano. |
| 4. | 06/07/2021 | Mazungumzo baina ya Rais ya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mhe. Charles Michel Rais wa Baraza la Ulaya na Mhe. Blinken, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani. | Mazungumzo hayo yalilenga juu ya uwezekano wa Serikali ya Tanzania kunufaika na msaada kutoka Umoja wa Ulaya katika kukabiliana na athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na Uviko -19. |
| 5. | 05 -07/07/2021 | Mkutano wa Mawaziri wa Kamati ya Asasi ya Ushirikiano katika siasa, ulinzi na Usalama | Kikao kilifanyika jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere. Lengo ni kujadili na kutoa utekelezaji wa masuala mbali mbali yanayohusu sekta husika. |
| 6. | 06/07/2017 | Kikao cha Mashirikiano baina ya Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar na Shirika la UNCDF. | Kikao kilifanyika jijini Dar es Salaam Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dododma. Lengo la kikao ni mashirikiano katika maeneo makuu matatu ambayo ni kujenga uwezo katika miradi inayosimamiwa katika Halmashauri na Manispaa ambayo inahusu miradi ya ujenzi wa masoko na vituo vya daladala; Uboreshaji wa miundo mbinu katika sekta ya maji hasa katika maeneo ya usimamizi wa mapato na mifumo ya kudhibiti mapato ya maji na Suala la wajasiriamali wadogo wadogo. |
| 7. | 09/07/2021 | Kikao cha wadau kwa ajili ya ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Burundi | Kikao kilifanyika jijini Dododma katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Kikao kililenga katika kupitia muhtasari wa masuala ya ushirikiano kati ya Tanzania na Burundi sambamba na kuainisha maeneo ambayo Tanzania ingependa kupewa kipaumbele katika ushirikiano wa nchi mbili hizo. |
| 8. | 16-20-23-<br>/07/2021<br>02/08/2021 | Kikao cha wadau kuhusu uwasilishaji wa vipaumbele kwa ajili ya USA na EU. | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Katika kikao hicho kilichoanzia katika ngazi ya |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | | Makatibu Wakuu na kufuatiwa na ngazi ya Wataalam kiliandaa maeneo ambayo yalipendekezwa kuwasilishwa USA na EU na hatimae kuwasilishwa ofisi ya Rais kwa ajili ya kuwasilishwa kunakohusika. |
| 9. | 14/08/2021 | Kikao cha Kamati ya kitaifa ya kusimamia masuala ya mikopo dhamana na misaada (NDMC) | Kikao kilifanyika Wizara ya Fedha na Mipango katika jengo la hazina jijini Dodoma. Katika kikao hicho Wajumbe walijadili miradi na maombi yaliyowasilishwa katika kikao. Katika mjadala huo Kamati ilipata fursa ya kukutana na wawakilishi wa miradi husika kutoka taasisi zinazosimamia miradi hiyo ambao walialikwa katika kikao hicho na hivyo kutoa maelezo ya kina juu ya miradi iliyowasilishwa kwa lengo la kuwajengea uelewa wajumbe na kuwa na taarifa za kutosha ili kufanya maamuzi ya miradi husika. Baada ya kupitia na kufanya maamuzi juu ya miradi na mapendekezo hayo Kamati iliandaa resolution kwa ajili ya kumbukumbu ya kikao husika na hatua za utekelezaji. |
| 10. | 19/08/2021 | Kikao cha utekelezaji wa maazimio ya kikao cha Mawaziri kilichofanyika tarehe 31/07/2021 | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kikao hicho kilichofanyika katika ngazi ya Wataalam kilipitia maazimio yaliyotolewa katika kikao cha ngazi ya Mawaziri na hatimae kuandaa babgo kitita kwa ajili ya uwasilishaji wa hatua za utekelezaji wa maazimio katika ngazi ya Makatibu Wakuu. |
| 11. | 03 -04/09/2021 | Mkutano wa kujadili mpango elekezi wa kupatiwa ufumbuzi na maagizo yaliyotolewa na wakaguzi wa Shirika la bahari duniani. | Kikao kilifanyika Kibaha – Mkoa wa pwani. Lengo ni kutoa taarifa kwa watendaji wakuu wa Wizara na Taasisi husika kwa upande zote mbili za Serikali ya Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania jinsi ya kuzipatia majibu hoja zilizotolewa na wakaguz hao. |
| 12. | 06 -10/09/2021 | Ziara ya Wataalamu wa Afya wa Italia katika sekta ya | Ziara ilifanyika jijini Dar es Salaam na Zanzibar. |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | Afya Tanzania. | Lengo ni kukagua na kuona changamoto ili Serikali ya Italia iweze kusaidia, hususan katika masuala ya wataamu wa Afya, vifaa vya tiba, kuboresha huduma za mama mjamzito na watoto. |
| 13. | 17/09/2021 | Mkutano wa kujadili rasimu ya hati ya makubaliano katika masuala ya kazi na ajira ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Umoja wa Famle za Kiarabu. | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika ukumbi wa Ngome, Ofisi ya Waziri Mkuu. Lengo ni kujadili na kufanya marekebisho ya rasimu hiyo kwa upande wa Tanzania. |
| 14. | 21 – 22/09/2021 | Kikao cha maandalizi ya mkutano wa 26 wa mabadiliko ya hali ya hewa. | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika hoteli ya Seint Petter. Katika kikao hicho wataalam kutoka katika sekta mbalimbali walipitia ripoti ya Mkutano wa 25 wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na kutathmini muendelezo wa utekelezaji wa maamuzi na maazimio ya mkutano uliopita pamoja na kuainisha vipaumbele vya kitaifa katika mabadiliko ya hali ya hewa. |
| 15. | 23 – 24/09/2021 | Kikao cha maandalizi ya mkutano wa 15 wa bioanuai (Biodivasity). | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katika hoteli ya Seint Petter. Katika kikao hicho wataalam kutoka katika sekta mbalimbali walipitia ripoti ya Mkutano wa 14 Bioanuai na kutathmini muendelezo wa maamuzi na miongozo ya mkutano uliopita pamoja na kuainisha vipaumbele vitakavyotoa mwelekeo wa Tanzania katika mkutano wa 15. |
| 16. | 28 -29/07/2021 | Kikao cha muongozo unaohusiana namna ya kukabiliana na uhalifu wa baharini na katika maziwa. | Kikao kilifanyika jijini Dodoma katka Ofisi ya Waziri Mkuu eneo la Relini kwa siku mbili ambapo siku ya pili kilifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.. Lengo ni kupitia muongozo huo ulioandaliwa na wataalam hao huko Bagamoyo, dhumuni la kuandaa muongozo huo ambao kimsingi |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | umekuwa na lengo la kuunganisha taasisi zote ambazo kwa njia moja au nyengine zinaguswa na suala la makossa ya uhalifu wa baharini na kwenye maziwa ili kuweza kuongeza ufanisi kwa taasisi hizo katika utendaji kazi wake pamoja kusaidia serikali katika kuimarisha usalama wa maeneo ya bahari pamoja na maziwa. |
| 17. | 27/09/2021 | Kikao baina ya Waziri wa Utalii wa Zanzibar na Balozi wa itali nchini Tanzania | Kikao kilifanyika jijini Dar es Salaam katika ofisi za Ubalozi wa Itali. lengo la kikao hicho ni kukuza mashirikiano katika Sekta ya Utalii hasa katika changamoto za kuzuiliwa watalii kutokana na UVIKO-19. |
| 18. | 28/09/2021 | Kikao hichi cha Kamati Tendaji ya Mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Programu ya Elimu ya Biashara kwa Vijana wa Afrika (ABE Initiative) kwa ajili ya batch ya tisa | Kikao kilifanyika katika hoteli ya Onomo Dar es Salaam. Lengo ni kupitia mapendekezo ya mchakato mzima wa kuchaguwa wanafunzi kwa ajili ya Mafunzo ya Shahada ya Uzamili nchini Japan kwa awamu ya tisa (9) ambayo imekuja baada ya kusitisha kwa muda sasa tangu 2019, kwa sababu ya kutokuwepo makubaliano baina Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan. |
| 19. | 14/07/2021 | Ripoti ya kikao baina ya Waziri Wa Elimu na Amali-Zanzibar na Balozi wa Canada Hapa Dar Es Salaam. | Kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam. Lengo ni kuimarisha mashirikiano baina ya Canada na Zanzibar na pia kuwapa mualiko kwenda Zanzibar |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | | kutembelea baadhi ya maeneo kwaajili ya kuangalia fursa mbalimbali kwa maslahi ya nchi. |
| 20. | 15 na 30/09/2021 | Kikao cha maandalizi ya kongamano la biashara kati ya Tanzania na UK | Kikao kilifanyika jijini Dar es Salaam. Lengo la kikao ni mataarisho ya kongamano hilo. |
| 21. | 21/09/2021 | Kikao cha wadau wa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kujiandaa na kongamano la biashara kati ya Tanzania na Uk | |
| 22. | 07/10/2021 | Kikao cha maandalizi ya sherehe za miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara. | Kikao husika kimefanyika Jijini Dodoma katika ukumbi wa Mikutano Afisi ya Waziri Mkuu Mlimwa. Kikao kilikua na lengo la kupitia mapendekezo ya shughuli zinazotarajiwa kufanyika katika maadhinisho ya sherehe za uhuru wa Tanzania Bara ambazo huadhimishwa kila ifikapo tarehe 09 Disemba. Kikao kimepitia na kujadili shughuli mbali mbali na hatimae kutoa maazimio kwa ajili ya utekelezaji. |
| 23. | 13/10/2021 | Kikao cha maandalizi ya mazungumzo ya kisiasa (Political dialogue) kati ya Tanzania na Umoja wan chi za Ulaya. | Kikao husika kimefanyika Jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa mikutano wa Julius Nyerere (JNICC). Kikao hicho kilikua na lengo la kufanya maandalizi ya mazungumzo ya pamoja kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya yanayotarajiwa kufanyika tarehe 29/10/2021 Jijini Dar es Salaam. |
| 24. | 18/10/2021 | Kikao cha Kamati ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe cha Maandalizi ya Sherehe za miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. | Kikao kimefanyika jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano ofisi ya Waziri Mkuu katika Mtaa wa Relini. Lengo la kikao husika ilikua ni kuwasilisha Bajeti na miradi kutoka katika taasisi zilizopangiwa kushiriki katika maandalizi ya shughuli zitakazofanyika katika maadhimisho ya sherehe za miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. |
| 25. | 06/11/2021 | Kikao cha Kamati ya maadhimisho ya Kitaifa ya sherehe za miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. | Kikao kimefanyika jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Waziri Mkuu Mlimwa. Lengo la |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | | kikao husika ni kupata taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali zilizopangwa kutekelezwa na taasisi husika kupitia maagizo ya kikao kilichopita. |
| 26. | 18/11/2021 | Kikao cha Kamati ya Wataalamu ya kusimamia masuala ya mikopo dhamana na misaada (TDMC) | Kikao kilifanyika Wizara ya Fedha na Mipango katika jengo la hazina jijini Dodoma. Kikao kilipitia jumla ya maombi 11yaliyowasilishwa na maombi 10 yalipitishwa kwa masharti ya kuzitaka taasisi husika kufanya marekebisho katika maandiko yao na hatimae kuyawasilisha kwa ajili ya maandalizi ya kikao cha NDMC. |
| 27. | 03/12/2021 | Kikao cha kupitia na kuthibitisha mpango kazi kati ya Tanzania na UNICEF kwa mwaka 2021-2022 | Kikao kilifanyika Wizara ya Fedha na Mipango katika jengo la hazina jijini Dodoma. Kikao hicho kilipitia mpango husika ambao umeandaliwa na kufanya marekebisho katika maeneo kadhaa kwa ajili ya kuwasilishwa UNICEF kwa utekelezaji. |
| 28. | 24/11/2021 | Ripoti Ya Mazungumzo Mafupi Kati Katibu Mkuu Wizara Ya Fedha Na Mipango Zanzibar Na Ya Ujumbe Kutoka Ubalozi Wa Ujerumani Tanzania. | Katika mazungumzo hayo ujumbe kutoka ubalozi wa Ujerumani umemueleza Katibu mkuu kuwa Serikali ya Ujerumani pamoja na Serikali ya Switzerland zipo tayari kutoa msaada ya huduma ya bima ya afya na wanachosubiri ni ruhusa kutoka upande wa Zanzibar kuanza mradi huo kwa hatua za mwanzo ambapo wata saini makubaliano juu ya hatua kwa hatua ya mradi huo. |
| 29. | 16 /11/ 2021 | Ripoti Kuhusu Kongamano La Biashara Na Uwekezaji Kati Ya Tanzania Na Uingereza Lililofanyika Tarehe 16 Novemba, 2021 Katika Ukumbi Wa Mkutano Wa Mwalimu Julius Nyerere (Jnicc) Jijini Dar Es Salaam | Malengo ya Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza ni yafuatayo;<br>i. Kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji uliopo baina ya Tanzania na Uingereza.<br>ii. Kujadili fursa za biashara na uwekezaji zilizopo katika nchi hizo mbili |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | pamoja na kuanisha changamoto zinazokwaza ufanyaji wa biashara na kuzitafutia suluhu.<br>iii. Kujadili miradi inayoendelea kutekelezwa baina ya Tanzania na Ungereza na kuangalia maeneo yenye fursa za kupatiwa misaada.<br>iv. Kupata fursa za ufadhili wa fedha kutoka makampuni na taasisi za kifedha kutoka Uingereza kwa wafanyabiashara kutoka Tanzania. |
| 30. | 5 /11/ 2021 | Ripoti Ya Kikao Baina Ya Waziri Wa Fedha Na Mipango Zanzibar Na Balozi Wa Uarabuni (Uae) Nchini Tanzania Kilichofanyika Katika Ofisi Ya Uratibu Shughuli Za Smz Dodoma | Lengo la kikao hicho ni kukuza mashirikiano kati ya Zanzibar na Falme za Kiarabu ambapo pamoja na mambo mengine kikao hicho kimegusia namna nchi za Falme za Kiarabu zinaweza kuisadia Zanzibar katika kutekeleza miradi na program zake tofauti ilizojipangia. |
| 31. | 24 /11/ 2021 | Ripoti Ya Ziara Ya Mhe. Waziri Wa Biashara Na Maendeleo Ya Viwanda Katika Kutembelea Kiwanda Cha Uzalishaji Wa Vifaa Vya Umeme 'Elsewedy Electric' Kilichopo Kigambo - Dar Es Salaam | Madhumuni makuu katika ziara hii ni kufanya mazungumzo na wawekezaji hao juu ya maeneo ya kuwekeza Zanzibar kwa vile wameonesha nia yao ya kuwekeza Zanzibar; na kutembelea kwenye uwekezaji uliofanya na Kampuni hiyo katika Mji wa Viwanda (Industrial Park) Kigamboni |
| 32. | 25-26/11/2021 | Mkutano wa majadiliano ya kimkakatati "Stratagic Dialogue"uliofanyika ukumbi wa Banki kuu ya Tanzania Dar es Salaam. | Lengo ni kujadili majadiliano ya kimkakati kati ya Serikali ya Washirikiano wa Maendeleo. |
| 33. | 3 /10/ 2021 | Ripoti Ya Ziara Ya Waziri Wa Wizara Ya Mawasiliano Na Uchukuzi Zanzibar, Watendaji Wake Na Wa Mamlaka Ya Mawasiliano Tanzania Hapa Dar Es Salaam Katika Vituo | Lengo ni kujifunza namna gani mawasiliano yanasafirishwa ndani na nje ya nchi na namna gani Serikali itafaidika kutokana na huo mradi kwa namna |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | Vinavyoshughulika Na Kupokea Na Kutoa Mawasiliano Nchini (Landing Station.) | moja au nyingine. |
| 34. | 16/11/2021 | Ziara Ya Kamati Ya Fedha Na Uchumi Ya Baraza La Wawakilishi Zanzibar na kutembelea Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC), Shirika la Bima la Zanzibar kanda ya Pwani ( Dar es salaam, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) tawi la Kiisilamu Lumumba, Benki kuu ya Tanzania (BoT), | Lengo ni kujifunza namna gani mashirika hayo yanafanyakazi pamoja changamoto wanazokabiliana nazo. |
| 35. | 14/12/2021 | Ripoti ya kikao cha mashirikiano baina ya Wizara ya Ardhi SMZ na SMT | Lengo ni kubadilishana uzoefu na kujifunza namna gani watatua changamoto zao. |
| 36. | 13-15/12/2021 | Kikao cha mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMT) na Wizara ya Ujenzi, mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) – sekta ya Uchukuzi kilichofanyika Mwanza | Lengo ni kujadili changamoto na kuzitatua pamoja na kuangalia fursa zilizokuwepo katika sekta sekta zisizo za Muungano. |
| 37. | 07/10/ 2021 | Ripoti Ya Kikao Cha Kongamano La Ushiriki Kati Ya Uturuki Na Afrika | Kikao hicho ambacho kilikuwa na agenda nne kuu baada ya utangulizi ambazo ni malengo ya kongamano, sekta za kipaumbele, faida ya kushiriki katika kongamanona mikakati ya uhamasishaji wa washiriki wa kongamano. |
| 38. | 18/10/2021 | Ripoti Ya Kikao Cha Wadau Kujadili Mwongozo Wa Kitaifa Wa Kukabiliana na Vitendo Vya Kihalifu katika Bahari na Maziwa Kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi Ya Waziri Mkuu - Dodoma | Lengo la kikao hicho ilikuwa kupokea maoni na ushauri kabla ya rasimu hiyo kuwasilishwa kwenye kikao cha Makatibu wakuu kwa ajili ya kuridhiwa. Kikao hicho pia kilijuulishwa hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa maeneo mengine ya Mradi wa Kukabiliana na Vitendo vya Kihalifu katika |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | | | Bahari na Maziwa. |
| 39. | 17 -21/ 01-2022 | Ziara ya mawasiliano, Ardhi na Nishati iliyofanyika katika jiji la Dar es Salaam kuanzia tarehe katika Ofisi za Shirika la nyumba Tanesco, Posta, Simu (TTCL) na DAWASA | Lengo ni kuonana na kujifunza kwa namna gani mashirikiano hayo yanavyofanya kazi zao za changamoto wanazokabiliana nazo. |
| 40. | 04/03/2022 | Kikao cha Serikali na Serikali (G2G) baina ya Serikali ya Uingereza na Tanzania kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Bunge mjini Dodoma. | Lengo ni kujadiliana utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano wa majadiliano ya kiserikali (G2G) kati ya Serikali ya Tanzania na Uingereza. |
| 41. | 28/12 -16/01/22 | Tamasha la biashara la zanzibar ya miaka 56 ya Mapinduzi ya Biashara ya mwezi wa January 2022 | Lengo kujitambulisha na kuitangaza Ofisi ya Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dododma. |
| 42. | 12/02/2022 | Ofisi ilishiriki ziara ya Kamati ya kilimo, biashara na utalii ya baraza la wawakilishi katika ofisi ya ZSTC zilizopo Dar es Salaam | Lengo ni kufuatilia uendeshaji wa shirika hilo kwa upande wa Tanzania bara pamoja na kukagua mali za shirika hilo. |
| 43. | 6-7/03/2022 | Ofisi ilishiriki kikao cha kwanza cha maandalizi ya majadiliano ya mkataba wa ubia wa kiuchumi (Economic Partnership Agreement EPA) baina ya nchi za Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) na umoja wa Ulaya (EU) | |
| 44. | 23 – 24. 02. 2022 | Ofisi ilishiriki kikao cha kumbukumbu Ya Kikao Cha Wadau Kwa Ajili Ya Kupokea Na Kujadili Maoni Ya Wadau Kuhusiana Na Uridhiaji Wa Mkataba Wa Eneo Huru La Biashara La Utatu (Comesa, Eac, Na Sadc) kilichofanyika katika Ukumbi Chuo cha Elimu ya Biashara [Collage of Business Education] (CBE) | |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 45. | 25/01/2022 | Ofisi ilishiriki Ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Kutembelea Shirika La Viwango Tanzania (Tbs) jijini Dar es Salaam. | Lengo ni kujifunza na kupata uzoefu wa namna shirika hilo linavyofanya kazi. |
| 46. | 31/01/2022 | Ofisi ilishiriki Mazungumzo Mafupi kati Waziri wa Fedha na Mipango Wa Serikali Ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Jamal Kassim na Ujumbe Kutoka Benki Ya Dunia na ujumbe kutoka Benki ya Dunia ukiongozwa na Mkurugenzi wa nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe Bi. Mara K. Warwick yalifanyika Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ –Dodoma. | Lengo kuu la mazungumzo hayo ni kujadili masuala mbali mbali ya maendeleo kupitia miradi inayodhaminiwa na benki ya dunia kwa upande wa Zanzibar pamoja na kupendekeza maeneo mapya ya miradi ya ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na benki ya dunia, kwa kuwa Tanzania ni nchi mwanachama ni wajibu wa benki hio kuhakikisha nchi wanachama wanakuza uchumi wao. |
| 47. | 01-04/02/2022 | Ofisi ilishiriki Ziara Ya Kamati ya Bajeti la Baraza La Wawakilishi- Tanzania Bara ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hio Mhe. Ali Suleiman Ameir katika Mamlaka ya Serikali Mtandao, Shirika la Nyumba la Taifa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Dar es salaam. | Lengo la ziara hio ni kujifunza na kubadilishana mawazo ya kiutendaji katika Taasisi hizo kwa nia ya kutatua changamoto za kiutendaji ili kuimarisha maendeleo ya Zanzibar. |
| 48. | 03/02 - 04/02/2022 | Ziara Ya Uongozi wa Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya kati Zanzibar (Smida) Katika Shirika La Kuhudumia Viwanda Vidogo Jijini Dar Es Salaam (Sido). | Lengo ni kujifunza namna SIDO wanavyotekeleza majukumu yao ambayo yanfanan na majukumu ya SMIDA. |
| 49. | 30/03/2022 | Ofisi ilishiriki ziara ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Uwekezaji Zanzibar pamoja na ZAWEMA (Wakala wa | Lengo ni kujifunza namna wakala hao wanavyofanyakazi kazi ili Zawema nao waweze |

| Nam. | Tarehe | Kazi Husika | Maelezo |
| --- | --- | --- | --- |
| | | Vipimo Zanzibar), na Wakala wa Vipimo Tanzania bara iliyofaanyika kibaha mkoa wa pwani. | kuboresha huduma zao |
| 50. | 31/03/2022 | Ofisi ilishiriki katika mazungumzo baina ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Uwekezaji Zanzibar na JICA yalifanyika ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma. | Lengo ni kuomba msaada wa kuendeleza sekta ya viwanda pamoja na kuwashawishi kwenda Zanzibar kwa ajili ya uwekezaji. |

KIAMBATISHO NAM.5

**Idadi ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mrefu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| JINA LA IDARA/TAASISI | CHETI (CERTIFICATE) | | STASHAHADA (DIPLOMA) | | SHAHADA YA KWANZA (DEGREE) | | STASHAHADA YA UZAMILI (PGD) | | SHAHADA YA PILI (MASTERS) | | SHAHADA YA UZAMIVU (PHD) | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M.ME | M.MKE | M.ME | M.MKE | M.ME | M.MKE | M.ME | M.MKE | M.ME | M.MKE | M.ME | M.MKE | |
| Afisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais | - | - | - | 1 | - | 1 | - | - | 2 | 1 | - | - | **5** |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1 | - | - | - | 3 | 3 | - | - | 1 | - | - | 1 | **9** |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | 3 | 1 | 1 | **6** |
| Idara ya Uratibu na Shughuli za Serikali | - | - | - | - | - | - | - | - | 3 | 5 | - | 1 | **9** |
| Afisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | 1 | - | - | **2** |
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | 1 | - | - | **2** |
| Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | - | - | - | - | 1 | 2 | - | - | - | - | - | - | **3** |
| Afisi Kuu - Pemba | 4 | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | **5** |
| **Jumla** | **5** | **-** | **-** | **1** | **4** | **8** | **-** | **1** | **7** | **11** | **1** | **3** | **41** |
| Baraza la Wawakilishi | - | - | 3 | - | 1 | 1 | - | - | 4 | 2 | - | 2 | **13** |
| Tume ya Uchaguzi | - | - | - | - | 2 | 3 | - | - | 1 | - | - | 1 | **7** |
| **JUMLA KUU** | **5** | **-** | **3** | **1** | **7** | **12** | **-** | **1** | **12** | **13** | **1** | **6** | **61** |

**Kiambatisho Nam. 6**

**Upandishwaji wa Madaraja kwa Wafanyakazi**

| Nam. | KIWANGO CHA ELIMU | JINSIA | CHEO/DARAJA ANALOTOKA | CHEO/DARAJA ALILOPANDISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Form III | MKE | Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la III | Afisa Utumishi Msaidizi Mwandamizi Daraja la II |
| 2. | Stashahada ya Ukatibu Muhtasi | MKE | Katibu Muhtasi Daraja la III | Katibu Muhtasi Daraja la I |
| 3. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MKE | Afisa Utumishi Msaidizi Mwandamizi Daraja la II | Afisa Utumishi Msaidizi Mwandamizi Daraja la I |
| 4. | Stashahada ya Ukatibu Muhtasi | MKE | Katibu Muhtasi Daraja la II | Katibu Muhtasi Daraja la I |
| 5. | STD VII | MKE | Muhudumu Daraja la III | Muhudumu Mwandamizi Darala la II |
| 6. | Form III | MKE | Afisa Ghala Daraja la II | Msaidizi Afisa Ghala Daraja la I |
| 7. | Form III | MKE | Muhudumu Daraja la III | Muhudumu Daraja la II |
| 8. | Stashahada ya Uongozi wa Biashara | MKE | Msaidizi Mkaguzi wa Ndani Daraja la II | Mkaguzi wa Ndani Daraja la I |
| 9. | Form II | MME | Muhudumu | Muhudumu |

| Nam. | KIWANGO CHA ELIMU | JINSIA | CHEO/DARAJA ANALOTOKA | CHEO/DARAJA ALILOPANDISHWA |
|---|---|---|---|---|
| | | | Daraja la III | Daraja la I |
| 10. | Form III na Mafunzo ya Udereva | MME | Dereva<br>Daraja la III | Dereva Mwandamizi<br>Daraja la I |
| 11. | Form IV | MME | Msaidizi Muhasibu | Msaidizi Muhasibu Mwandamizi Daraja la II |
| 12. | Stashahada ya Manunuzi na Ugavi | MME | Afisa Ugavi na Manunuzi Daraja la III | Afisa Ugavi na Manunuzi Daraja la II |
| 13. | Stashahada Utawala wa Umma | MME | Afisa Uendeshaji na Utumishi Daraja la II | Afisa Utumishi Msaidizi Mwandamizi Daraja la II |
| 14. | Form III | MME | Msaidizi Mwangalizi wa Afisi Daraja la II | Msaidizi Mwangalizi wa Afisi Daraja la I |
| 15. | Form IV | MME | Dereva mwandamizi Daraja la II | Dereva mwandamizi Daraja la I |
| 16. | Stashahada ya uhifadhi kumbukumbu | MKE | Afisa Kumbukumbu Msaidizi Siri Daraja la II | Afisa Kumbukumbu Mwandamizi Daraja la II |
| 17. | Stashahada ya uhifadhi kumbukumbu | MKE | Afisa Kumbukumbu Bayana Daraja la II | Afisa Kumbukumbu Msaidizi Mwandamizi Daraja la II |
| 18. | Form II | MME | Taarishi Mwandamizi Daraja la I | Taarishi Mwandamizi Daraja la II |

| Nam. | KIWANGO CHA ELIMU | JINSIA | CHEO/DARAJA ANALOTOKA | CHEO/DARAJA ALILOPANDISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 19. | Form II | MME | Taarishi Mwandamizi Daraja la I | Tarishi Daraja la I |
| 20. | Stashahada ya Manunuzi na Ugavi | MME | Afisa Mtunza Ghala Msaidizi Daraja la III | Afisa Mtunza Ghala Msaidizi Daraja la II |
| 21. | Form II | MME | Mpishi Daraja la II | Mpishi Daraja la I |
| 22. | Form II | MME | Dereva Daraja la III | Dereva Daraja la I |
| 23. | Shahada ya Kwanza ya Utawala wa Umma | MME | Afisa Mipango Daraja la II | Afisa Mipango Daraja la I |
| 24. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MME | Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la II | Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la I |
| 25. | Stashahada ya Uhusiano wa kimataifa | MME | Mpiga Chapa Msaidizi Daraja la II | Mpiga chapa Daraja la I |
| 26. | Shahada ya Kwanza ya Rasilimali Watu | MME | Afisa Uratibu Daraja la II | Afisa Uratibu Daraja la I |
| 27. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MME | Afisa Uratibu SMZ Msaidizi Daraja la II | Afisa Uratibu SMZ Msaidizi Mwandamizi Daraja la I |
| 28. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MKE | Katibu Muhtasi Mwandamizi Daraja la II | Katibu Muhtasi Mwandamizi Daraja la I |
| 29. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MME | Afisa Uratibu Msaidizi wilaya Daraja I | Afisa Uratibu Msaidizi Mwandamizi wilaya |

| Nam. | KIWANGO CHA ELIMU | JINSIA | CHEO/DARAJA ANALOTOKA | CHEO/DARAJA ALILOPANDISHWA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Daraja II |
| 30. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MKE | Afisa Sherehe Msaidizi Daraja la II | Afisa Sherehe Msaidizi Daraja la I |
| 31. | Stashahada ya Rasilimali Watu | MKE | Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la II | Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la I |
| 32. | Stashahada ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano | MKE | Katibu Muhtasi Daraja I | Katibu Muhtasi Mwandamizi Daraja II |

Kiambatisho Nam. 7

**Mikutano Iliyohudhuriwa Inayohusu Shughuli za Uchaguzi**

| NO. | AINA YA MKUTANO | ALIYEHUDHURIA | PAHALA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kikao kilichoandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa. | Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya ya Zanzibar pamoja na Mkurugenzi wa Uchaguzi. | Dodoma – Tanzania. |
| 2. | Mkutano Mkuu wa Mwaka, wa Kuadhimisha miaka 23 ya Tume za Uchaguzi za Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (ECF- SADC). | Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Mjumbe mmoja wa Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi pamoja na Mkuu wa Kurugenzi ya Mipango na Utawala. | mkutano huo uliendeshwa kwa njia ya mtandao (online). |
| 3. | Mkutano wa kujadili utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Asasi za Kiraia yaliyotolewa katika ripoti za Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2020. | Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilikutana na Asasi za Kiraia (Jumuiya ya Kupambana na Changamoto za Vijana Zanzibar"Zanzibar Fighting Against Youth Challenges"-ZAFAYCO na Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar-JUWAUZA). | Maisara –Zanzibar. |
| 4. | Mkutano wa kujadili vipaumbele vya Tume vinavyoweza kutekelezwa kwa mashirikiano na UNDP katika Programu za UNDP ya miaka mitano ijayo. | Mshauri Mwelekezi pamoja na Afisa Uendeshaji wa Shughuli za Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Program-UNDP) na Watendaji wa Afisi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | Maisara –Zanzibar. |

| NO. | AINA YA MKUTANO | ALIYEHUDHURIA | PAHALA |
|---|---|---|---|
| 5. | Mkutano wa kujadiliana juu ya uwezekano wa kushirikiana katika kuzipitia na kuzifanyia marekebisho Sheria za Uchaguzi za Zanzibar ili kuondoa changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. | Watendaji wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Mkurugenzi Mkaazi wa Taasisi ya Kimataifa ya 'International Republican Institute'-IRI. | Maisara –Zanzibar. |
| 6. | Mkutano wa kujadiliana juu ya uwezekano wa kushirikiana katika nyanja mbali mbali ikiwemo utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, | Mwakilishi Mkaazi wa UNDP Tanzania pamoja na Watendaji wa Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. | Maisara –Zanzibar. |
| 7. | Kikao cha siku tano juu ya utaalamu katika kuendeshesha uchaguzi (Elections Profession) kwa nchi za Jumuiya ya Madola (Commonwealth). | Afisa Uchaguzi Wilaya ya Mkoani | Ghana. |
| 8. | Mafunzo ya wiki moja ya Uangalizi wa Uchaguzi wa Muda mrefu kwa Maafisa Tehama (ICT-BASED LONG-TERM ELECTION OBSERVATION) yaliyodhaminiwa na Sekretarieti ya Jumaiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-SECRETARIAT). | Watendaji wawili wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (Mkuu wa Divisheni ya Usimamizi wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Afisa TEHAMA | Botswana. |

Kiambatisho Nam. 8

**Taarifa ya Upatikanaji wa Fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa Kipindi Cha Julai, 2021 Hadi Machi, 2022**

| S/N | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 1,825,256,455 | 1,462,144,921 | 820,516,570 | 56 | 45 |
| 2 | Uratibu wa Shughuli za Serikali | 2. Kukabiliana na Maafa | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 1,387,000,000 | 1,265,650,000 | 635,718,259 | 50 | 46 |
| | | 3. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 1,243,681,493 | 1,175,188,620 | 874,318,862 | 74 | 70 |
| | | 4. Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ | 689,096,781 | 507,957,648 | 368,578,145 | 73 | 53 |
| | | | Ruzuku kwa ajili ya Shughuli za Idara ya Uhamiaji | 16,118,600,000 | 12,088,950,003 | 4,200,000,000 | 35 | 26 |

| S/N | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 5. Shughuli za SMZ Dar es Salaam | Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, Dar es Salaam | 671,107,912 | 512,736,182 | 361,397,289 | 70 | 54 |
| 3 | Uendeshaji na Uratibu | 6. Uongozi na Utawala | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,571,839,909 | 1,206,014,305 | 852,250,923 | 71 | 54 |
| | | 7. Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 450,331,485 | 340,218,584 | 199,372,312 | 59 | 44 |
| | | 8. Ofisi Kuu Pemba | Ofisi Kuu Pemba | 764,092,544 | 584,812,540 | 583,353,080 | 100 | 76 |
| 4 | Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | 9. Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | Baraza la Wawakilishi | 24,337,975,465 | 17,608,161,763 | 12,844,441,918 | 73 | 53 |
| 5 | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | 10.Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | | | | | | |

| S/N | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 11. Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba | | | | | | |
| 6 | Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi | 12.Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | Tume ya Uchaguzi | - | | - | | - |
| 7 | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 13. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Unguja | | 2,248,900,000 | 1,767,683,812 | 1,338,644,440 | 76 | 60 |
| | | 14. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Pemba | | | | | | |
| | **JUMLA** | | | **51,307,882,044** | **38,519,518,378** | **23,078,591,798** | **60** | **45** |

**Kiambatisho Nam. 10**

## Ukusanyaji Mapato kwa Kipindi cha Julai 2021 – Machi, 2022

| IDARA/TAASISI | FEDHA ILIYOTENGWA | FEDHA ILIYOPANGWA KUSANYWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOKUSANYWA MIEZI TISA | ASILIMIA MIEZI TISA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|
| Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 49,422,100 | 40, 022,000 | 22,065,000 | 55 | 45 |
| Ofisi Kuu Pemba | 21,180,900 | 15,389,900 | 2,940,000 | 19 | 14 |
| Tume ya Uchaguzi | 100,712,000 | 80,709,000 | 402,000 | 0.49 | 0.4 |
| **JUMLA** | **171,315,000** | **136,120,900** | **25,407,000** | **19** | **15** |

**DEKiambatisho Nam. 11**

**Makadirio ya Fedha kwa Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2022 / 2023**

| IDARA/TAASISI | MSHAHARA | 0/C | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO WAHISANI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| Faragha | 825,383,836 | 882,683,290 | | | **1,708,067,126** |
| Maafa (Washirika) | - | 459,142,758 | - | - | **459,142,758** |
| Sherehe | 216,700,920 | 1,064,290,361 | | | **1,280,991,281** |
| Uratibu Smz | 434,505,528 | 298,017,140 | 100,000,000 | 14,644,434,250 | **15,476,956,918** |
| Uratibu Dodoma | 417,850,560 | 740,711,481 | | | **1,158,562,041** |
| Utumishi | 663,534,672 | 965,715,128 | | | **1,629,249,800** |
| Mipango | 186,898,860 | 298,850,241 | | | **485,749,101** |
| Pemba | 634,485,624 | 290,589,601 | | | **925,075,225** |
| **Jumla Ndogo** | **3,379,360,000** | **5,000,000,000** | **100,000,000** | **14,644,434,250** | **23,123,794,250** |
| **Ruzuku** | | | | | |
| Maafa | 479,700,000 | 755,000,000 | | | **1,234,700,000** |

| IDARA/TAASISI | MSHAHARA | 0/C | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO WAHISANI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| Uhamiaji | | 16,119,200,000 | | | **16,119,200,000** |
| **Jumla Ndogo** | **479,700,000** | **16,874,200,000** | **-** | **-** | **17,353,900,000** |
| **Jumla Kuu** | 3,859,060,000 | 21,874,200,000 | 100,000,000 | 14,644,434,250 | **40,477,694,250** |
| Baraza La Wawakilishi | 8,940,194,460 | 15,734,505,540 | | | **24,674,700,000** |
| Tume Ya Uchaguzi | 1,412,600,000 | 803,930,000 | | | **2,216,530,000** |
| **Jumla Kuu OMPR** | **14,211,854,460** | **38,412,635,540** | **100,000,000** | **14,644,434,250** | **67,368,924,250** |